

KANISA LIKICHAGUA

SHERIA BADALA YA NEEMA

 Isitoshe, wakati mwingine pasipo na upako juu ya watu wanashindwa kulipata. Nina furaha sana, usiku wa leo, kuwa hapa katika ushirika pamoja nanyi nyote waaminio, na ndugu yetu mchungaji mpendwa hapa, Ndugu Sullivan, ndugu mpendwa, tukiomba leo pamoja, na kuzungumza.

² Wengi wamekuwa wakipiga simu siku nzima, kwa, wahudumu mbalimbali, mahali mbalimbali, wakitaka kuwa na, kuondoka hapa kuhudhuria mkutano mwingine, ama mahali fulani, lakini sijatulua tangu Krismasi, nami ninachoka sana. Kila mtu anajua nina kama siku sita au saba za kupumzika, kwa hiyo sina budi kuwa nazo, karibu nimekwisha.

³ Pia, mwajua, ndio kwanza tuondoke kwenye mkutano ambapo kadiri ya maono thelathini katika usiku mmoja, hakuna mtu atakayejua hilo linamaanisha nini, ni, hiyo itakuwa ni siri itakayoenda kaburini pamoja nami, na Mungu. Wangeweza tu... Wewe... Hakuna njia ya kulielezea. Wewe tu, kuna ninii tu, kamwe huwezi kufanya hivyo. Wala hakuna ajuaye... Kama... Wazieni tu jambo hili: ono moja kutoka kwa Bwana wetu Yesu Naye akasema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” Mwanamke alingusa. Sasa, vipi kuhusu mwenye dhambi basi, ambaye ameokolewa kwa neema? Kitu pekee kinachofanya hivyo: “Nyingi kuliko hizi mtafanya,” ni ahadi, “kwa kuwa naenda kwa Baba.”

⁴ Na huyo hapo binti mkwe wangu, wakati alipokuwa kwenye safari hii ndefu ya mwisho, ya majuma manane, aliporudi nyumbani, alilala kitandani siku tatu ama nne apate tu kupumzika, kasema alikuwa karibu na kufa. Vema, hao wavulana, wote karibu wamefifia kwa uchovu. Nilikuja nyumbani, na kabla sijatoa nusu ya masanduku yangu, mimi huyu hapa ninaenda, ninaenda, ninaenda, ninaenda, ninaenda siku nzima, usiku kucha, na kwenda, kwenda, kwenda, mchana kutwa na usiku, na kuendelea tu namna hiyo, kwenda, na kwenda na kwenda.

⁵ Ndipo nikasema, “Vema, sasa unafikiri ni vigumu kuzunguka tu, kusimama tu mikutanoni, kisha kushuka, kuketi mikutanoni, kuufurahia, kwenda nyumbani, kwenda kulala, kulala nusu ya kesho yake ukitaka, kuamka, kisha kuhudhuria mkutano unaofuata, ndipo unachoka, unachukua tu jukumu la mmoja wa mikutano hiyo mabegani mwako, na kujua ya kwamba unawajibika kwake, unaona, kuwajibikia

kila kitu, kisha uhubiri,” wakati dakika ishirini za kunena kwa ushawishi zinalinganishwa na saa nane za kazi ngumu, ndivyo sayansi inavyosema, kwa mwili wako; wakati mwingine ninahubiri saa moja na nusu, saa mbili.

⁶ Isitoshe, ono moja litakurarua kuliko vile siku tatu za kuhubiri zingefanya. Unaona? Halafu unapata thelathini za hayo usiku mmoja. Unaona? Mnaona, hakuna njia, ni ninii tu, ni mwujiza, wenyewe ni mwujiza wa kipekee, kwamba Mungu hunijalia kuishi, na Yeye hufanya hivyo kwa ajili ye—yenu.

⁷ Ni wangapi waliopata kusikia juu ya Raymond Richey, Ndugu Raymond Richey? Hakuna. Los Angeles hivi majuzi usiku, alipiga magoti karibu nami, na kuomba. Mnajua Richey, Ndugu Richey yuko...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mlijua hilo? [Sehemu tupu kwenye kanda.] ...mbaya sana, ikamwingiza katika kupooza. Alifikiri angeweza tu kufanya mengi kama huyo mwingine, kwa hiyo akaondoka, na kuingia kwenye umishenari, kisha akarudi, na kuanzisha uamsho, naye amekwisha, akashikwa na kiharusi, fadhaa, naye ni, loo, yeye ni mahututi; na maskini ndugu mzuri sana.

⁸ Aliingia, mara aliponiona alijaribu kuzungumza, kisha akapiga magoti, nami nilikuwa nikijaribu kuelewa yale aliyosema, akasema, “Ndugu Branham, usiendeleo kwenda hivyo.” Kasema, “Usiendeleo kwenda, utakuwa kama mimi moja ya siku hizi, usifanye hivyo. Ninii tu...” Lakini nadhani labda bidii yetu huiteketeza hekima yetu, kwa hiyo tunaendelea tu kwenda kwa vyovyote vile, tukitumainia Bwana ya kwamba—ya kwamba itakuwa sawa.

⁹ Nina furaha sana kuwaona baadhi ya marafiki zangu humu ndani, usiku wa leo. Nanii wetu, katibu wangu wa kibinafsi, Ndugu Maguire na mkewe...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...kutoka Canada, Saskatchewan, nami nina furaha kuwa nao humu. Na ndugu zangu wawili hapa, kutoka huko chini Kentucky, kamwe siwezi kukumbuka majina yao. Wao ni...[Sehemu tupu kwenye kanda.] Ninaamini kweli mnatoka Arkansas, sivyo, ndugu? Nanyi mnakuja mikutanoni. Nami ninamwona Ndugu yangu Dauch, ama *Dauch*, Dauch aliyeketi hapa nje kutoka, anatoka hapa Ohio, na mke wake mpendwa nyuma yake, pale. Nina furaha sana kuwaona ninyi nyote humu, usiku wa leo, na watu mbalimbali safarini. [Sehemu tupu kwenye kanda.] Ninatambua, Ndugu Charlie, na Rodney, na Rogers, Ndugu Sothmann. Nami naele-...[Sehemu tupu kwenye kanda.]...usiku wa leo, baadhi, Billy alikuwa akiniambia alasiri ya leo. Nina furaha sana kwamba yupo hapa kutoka huko chini kabisa katika Georgia hiyo yenye jua kali. Baadhi yao walisema, “Unaendeleaje?”

¹⁰ Kasema, “Ninaganda.” Lakini tunaninii...Uko wapi, Ndugu Welch? Siwezi kukutambua, ninii kidogo tu...Mbona,

ameketi papa hapa chini ya uso wangu hapa, na Dada Evans. Naam, angalieni hapa, kundi kutoka Georgia kule. Hilo ni sawa, nina furaha kuwa nanyi nyote hapa ndani.

¹¹ Sasa, Bwana daima ambariki Ndugu Sullivan kwa kutualika hapa. Anajitwika mwenyewe udhamini, chini ya Mungu, kuninii... Nafikiri, ninyi watu, kama ninavyosikia, Ndugu Sullivan atawaacha hivi karibuni sana, akiondoka. Nanyi mtamkosa mtu maarufu. Mtu atakayejitokeza huko mbele ya umma kudhamini mkutano kama huu, mnaona, inaonyesha ya kwamba anawapenda, anajaribu kufanya jambo fulani kwa ajili ya watu, la sivyo asingeudhamini. Hiyo ni kweli. Mtumishi halisi wa kweli wa Mungu, mwaminifu kwelikweli. Ninamthamini Ndugu Sullivan kwa moyo wangu wote.

¹² Mtu apataye kuwa chochote ni mtu anayesimama peke yake, yeye na Mungu pekee, mtu ndiye huyo.

Kuna, kwenye Barabara ya Yeriko kuna nafasi
ya watu wawili tu
Si zaidi wala pungufu ni Yesu tu na wewe.
(Hivyo tu.)

¹³ Na kwa hiyo hivyo ndivyo inavyotubidi kutembea kwenye njia hii nyembamba, kila mtu aliyewahi kumfanyia Mungu lolote alipitia barabara iyo hiyo. Hiyo ni kweli. Kukosolewa, kuachwa, kutupwa nje, kupitia nyakati zote, vipindi vyote, imewabidi kutesewa jambo lile lile. Kwa hiyo, sisi ni kama tu walivyo, jambo lile lile, hatuna budi kusimama peke yetu. Lakini si peke yetu, Yeye daima yupo.

¹⁴ Tunawathamini wa—watu wanaosimamia ghala hili la silaha hapa, ambao huturuhusu kuwa na ghala hili la silaha, pia. Kama wako mahali wanapoweza kuisikia sauti yangu, hakika ninathamini ukarimu huu wenu ninyi wanaume, Bwana awabariki daima. Ni, sasa, ni Jeshi la Marekani, nasi tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki sana, na kuwasaidia.

¹⁵ Nami nawaambia tuko kwenye mpango wa kujihami, tunajua hilo, pamoja na mataifa mengine, na kadhalika, na kujaribu kuwashinda katika mashindano ya makombora. Ndugu zangu, kuna mbio moja ambayo hatuna budi kukimbia, hiyo ni mbio ya kutoka utotoni hadi kaburini, huku uso wetu ukiwa Kalvari, hiyo ndiyo mbio, hiyo ndiyo ngome yetu, ni hapo Kalvari.

¹⁶ Nipe kila askari Marekani aliyewekwa wakfu kwa Mungu, ameinamisha uso wake akiomba, nanyi mnaweza kulipua makombora yote, na kuyaachilia. Hiyo ni kweli. Tutakuwa tumelindwa salama sana hata kila taifa chini ya Mbingu litatuogopa, kama ilivyokuwa katika siku za Sulemani. Ninaamini nilihubiri juu ya hilo mara ya mwisho hapa juu, *Malkia wa Kusini*, jinsi ambavyo Israeli hawakuwa na matatizo

siku hizo na mataifa mengine yoyote, wote waliwaogopa, walimtumainia Bwana.

¹⁷ Siamini mnanisikia vizuri sana, kuna kurudishwa mwangwi huko? Mnaweza kuisikia huko nje vizuri, huko nyuma kabisa? Nilifikiri ilisikika kama kurudishwa mwangwi. Hebu tuone kama ninaweza kuibadilisha hii. Hiyo ni bora zaidi? Mnaweza kusikia hiyo vizuri zaidi, huko nyuma kabisa? Hakuna mtu anayesogea. Mnaweza kusikia hii vizuri zaidi hapa? Ninaamini nilivunja mimbara yangu. Vipi hiyo? Hiyo ni bora zaidi? Vema, tutajaribu kuiachia hapo.

¹⁸ Sasa, tunataka kuliendea Neno upesi. Niliwachelewesha jana usiku kwenye kanisa la Ndugu Sullivan, lakini sisi... Nilifurahia hasa kile Bwana alichotupa juu ya sauti, *Sauti Zisizojulikana*. Nasi tulijaribu kuelezea sauti nyingi zisizojulikana za siku hizi.

¹⁹ Ndipo basi, baada ya kumalizana na sauti zote zisizojulikana, ndipo tukaleta sauti ambayo ilikuwa ya hakika (Asante, Ndugu Gene, labda hilo litasaidia—litatusaidia tu kidogo. Vema.), juu ya sauti fulani za siku hizi. Nasi tuliona ya kwamba kulikuwa na sauti moja iliyokuwa ya hakika, hiyo ilikuwa ni sauti ya Injili. Na jinsi Injili ilivyokuja, si katika Neno pekee, bali kwa nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu. Sauti ile iliyokuja kwenye Siku ya Pentekoste kama upepo wa nguvu ukienda kasi, hiyo ilikuwa ni uhakika ya kwamba Uzima ulikuwa umekuja, kwa kuwa ulikuwa ni Uzima wa kiroho.

²⁰ Mnaweza kunisikia vizuri zaidi nikirudi nyuma? Niirudishe nyuma? Vema. Nitajaribu kuchukua baadhi ya mawazo ya Paul Rader. Ni wangepi waliowahi kumwona Paul? Nilimcheka Paul, alizoea kurudi nyuma sana, namna *hii*, daima akivuta suruali yake, ndipo angetoa hoja yake, na kukimbia moja kwa moja kuelekea jukwaani upesi alivyoweza na kutupa mikono yote miwili juu. Na kwa hiyo, angeenda mbali sana na maikrofoni yake.

²¹ Naam, imetokea nimemwona Ndugu na Dada Collins wameketi hapa nyuma kwenye kusanyiko. Mtu fulani asiyeamini ya kwamba Mungu huwapa wahubiri wa Kimethodisti ubatizo wa Roho Mtakatifu, huyo hapo ameketi mmoja ambaye Yeye alimpa ubatizo wa Roho Mtakatifu, mhubiri Mmethodisti, mhubiri Mmethodisti wa Kentucky anayempokea Roho Mtakatifu, na mtumishi mnyenyekevu wa Mungu sasa. Kwa hiyo tuna furaha kwamba Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya mtu yeyote anayemtaka. Mtu yeyote aliye tayari kuyafikia masharti ya Mungu anaweza kumpokea Roho Mtakatifu. Naam, ni kwa ajili ya Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri, Mlutheri, Mkatoliki, Myahudi, Mprotestanti, wa manjano, mweusi, mweupe, wa hudhurungi, na asiyejali, sisi sote pamoja, Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya wote.

²² Sasa, nataka kuinama, kama mtaviinamisha vichwa vyenu, kwa dakika chache tu, tunapoomba. Na kabla ya maombi, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kama una haja maalum, utaifanya ijulikane unapomwinulia Mungu mikono yako? Shikilia tu haja yako moyoni mwako. Mungu awabariki. Mungu na ampe kila mmoja wenu haja yake.

²³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia kiti Chako cha neema, sio kiti Chako cha haki, Bwana, tusingeweza kukistahimili, hatuombi haki, tungepotea, bali tunaomba neema. Nasi tunakuja kwa sababu Wewe umetuagiza tuje, nasi tunayo ahadi ya kwamba tutapokea kile tuombacho kama tutakuja kwa ujasiri, bila kutilia shaka, na kuomba katika Jina la Bwana Yesu, kwa kuwa imeandikwa, "Lolote mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Yesu." Yeye alisema, Mwenyewe, alipokuwa duniani, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya."

²⁴ Nasi tuna hakika ya kwamba tutapata kile tuombacho, kwa kuwa tunakuja kwa imani tukiamini kwa yote yaliyo moyoni mwetu ya kuaminia, nasi tunaomba, katika Jina la Yesu, ili neema, na rehema, na ujasiri zituzunguke, usiku wa leo, na kutupa sehemu kubwa ya Roho Wako moyoni mwetu tunavyomhitaji.

²⁵ Wape imani wale walioinua mikono yao, nami ni mmoja wao, kwa ajili ya haja iliyokuwako moyoni mwetu, kwamba tutaamini kwa mioyo yetu yote ya kwamba utatujalia haja yetu. Kwa kuwa tunaikabidhi ibada hii pamoja na sisi wenyewe Kwako ufanye nasi uonavyo kuwa inafaa, tunapolikaribia Neno kulihubiri, jalia Roho Mtakatifu aje na kuyatia maneno mafuta, na kuyapanda katika moyo wetu sote. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁶ Sasa, ninyi mnaoandika, kwa kawaida, Maandiko, Nitawaomba, usiku wa leo, mfungue Kitabu cha Kumbukumbu la Torati na mlango wa 2 na kifungu cha 3 kwa ajili ya somo:

Mlivyokaa kwenye mlima huu vyatosha: geukeni upande wa kaskazini.

²⁷ Ninapenda kufundisha kutoka kwenye Agano la Kale, kwa sababu Agano la Kale ni mfano wa lile Jipya. Na tunapoliendea fungu hili takatifu sana, usiku wa leo, kama vile Neno Lake lote lilivyo takatifu na lenye uchaji, ningependa kulinganisha mambo ya siku zilizopita ya Agano la Kale na Jipya, na siku zilizopo sasa.

²⁸ Israeli wasingeamini, kama mtu fulani angaliwaambia, kwamba walikuwa miaka arobaini kutoka kwenye nchi ya ahadi walipokuwa wakiimba, wakupaza sauti, na kucheza katika Roho upande wa pili wa Bahari ya Shamu. Hawangeamini kamwe kama mtu fulani angesema, "Mmetoka katika ile dhiki sasa, na yale mateso, Mungu amewakomboa, kisha akawavusha. . ." Nao

hawakuwa mbali ila safari ya siku chache tu, lakini, hata hivyo, kutokuamini kwao kuliwaweka jangwani kwa muda wa miaka arobaini. Nao baba zetu walifikia mahali pale pale yapata miaka arobaini iliyopita, ama zaidi kidogo, hali ile ile ilikuwako.

²⁹ Israeli walikuwa na uamsho mkuu, nao walikuwa wakienda zao kwe—kwe—kwenye nchi ya ahadi, ambako Mungu alikuwa ameapa kwamba angewapeleka, kwa baba Ibrahimu. Nao walikuwa wakienda kwenye nchi hii ya ahadi pamoja na ahadi za Mungu, baraka juu yao, nayo saa ya ukombozi ilikuwa imekaribia, naye Mungu alikuwa amefanya yote aliyokuwa ameahidi kufanya, nao walikuwa njiani mwao kwenda kwenye nchi hiyo.

³⁰ Haikuwa ila maili chache tu, ipime kwenye ramani, kwa kweli ninaamini ya kwamba ningeweza kuitembea chini ya siku tano, mimi mwenyewe, niondoke tu na kuitembea katika muda wa siku tano, kutoka Bahari ya Shamu hadi mahali walipovukia Yordani kuingia Palestina. Safari ndogo tu, na hata hivyo, kwa sababu ya kutokuamini kwao, iliawaweka miaka arobaini nyikani.

³¹ Sasa, hilo ni jambo zito, tunapaswa kulitafakari kwa muda kidogo. Hawakuamini hata kidogo kwamba kulikuwako na... maji ya Mara yalikuwa mbele yao, ama nyika ya Sini, ama Mlima Sinai, ama Kadeshi-Barnea, ambako walimkosea Mungu kabisa, wakati kutoka Kadeshi kulikuwa na siku kumi na moja tu mpaka kuvuka. Wasingeweza kuamini hilo, kwa sababu tayari walikuwa wameona mambo mengi sana makuu yakifanyika, walikuwa na hakika ya kwamba walikuwa katika mapenzi ya Mungu, kama tu vile baba zetu walivyokuwa miaka michache iliyopita. Nao walikuwa, lakini hapo ndipo walipofanya kosa lao kubwa, baya sana.

³² Wao, kosa kubwa sana ambalo Israeli waliwahi kufanya ni wakati walipoikana neema na kuikubali torati. Walifanya kosa lao kubwa kuliko yote katika Kutoka 19, lilikuwa ni moja ya makosa mabaya sana ambayo Israeli walifanya. Agano ambalo Mungu alifanya na Ibrahimu lilikuwa ni la neema tupu. Lakini neema ilikuwa imewapa mkombozi, nabii, mwana-kondoo wa sadaka, ilikuwa imewapa uamsho mkubwa sana waliopata kuwa nao, na hata hivyo, hawakuridhika nao, walitaka jambo ambalo wangeweza kubishania, walitaka mahali ambapo wangeweza kuwa na cha kufanya katika jambo hilo.

³³ Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa miaka arobaini iliyopita kwa baba zetu, baba zetu wa Kipentekoste, neema ilikuwa imewapa uamsho, pia ilikuwa imewatoa ulimwenguni, na kutoka kwenye machafuko walimokuwamo, katika madhehebu yao ya kawaida, na mashirika, na kadhalika, na ilikuwa imewaleta kwenye uamsho mkubwa sana waliowahi kuwa nao, ikawamwagia

Roho Mtakatifu, ikawajaza na Roho, walikuwa wakiimba, wakicheza katika Roho, wakiwa na wakati mzuri sana, wala hawakujua hata kidogo ya kwamba walikuwa na miaka hii yote mbali na ile ahadi kamili.

³⁴ Lakini kama ilivyokuwa kwa Israeli ya kawaida, ndivyo ilivyo na Israeli ya kiroho. Sisi ni Waisraeli kwa sababu sisi ni Uzao wa Ibrahimu, *huyo* Mwisraeli si yule aliye wa mwili, bali yule wa Roho. “Sisi tukiwa tumekufa katika Kristo tunachukua Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi pamoja na Ibrahimu sawasawa na ahadi.” Kwa hiyo sisi ni . . . Wala Ibrahimu hakuwa Myahudi, Ibrahimu alikuwa Mmataifa kutoka katika nchi ya—ya Wakaldayo, na mji wa Uru, alikuwa Mmataifa kabisa.

³⁵ Sasa, angalieni, lakini walikuwa *mbali* sana hivi kwa sababu walikataa kukubali kile Mungu alikuwa amewapa, nao walitaka kuongeza kitu fulani kwake. Hapo ndipo daima tunafanya makosa yetu, ni wakati tunapojaribu kuongeza jambo fulani kwenye yale Mungu amefanya, na yale Mungu amesema, achana tu nayo. Wametumia miaka elfu mbili wakijaribu kuongeza neno moja kwenye Sala ya Bwana kuiboresha, ama kuondoa Neno moja kuiboresha, wala huwezi kufanya hivyo, kwa sababu Yeye anaponena Hilo ni kamilifu, na ukiongeza chochote zaidi kwa ukamilifu umekiuka utaratibu. Mungu anapofanya lolote, ni kamilifu.

³⁶ Basi tunapojaribu kuwazia ya kwamba Yeye anahitaji msaada wetu, hahitaji msaada wetu, Yeye ni Mungu. Mnasema, “Vema, hana budi kuwatumia wanadamu kulihubiri Neno.” Kama tu vile Yohana alivyosema, “Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Yeye hatuhitaji. Yeye ni Muumba, anaweza kufanya lolote atakalo kwa sababu Yeye ni Mungu.

³⁷ Sasa, tunaona ya kwamba, mambo haya yote, waliandaa mwana-kondoo wa Pasaka, Mungu alikuwa amewapa mana kutoka Mbinguni kwa ajili ya safari yao, alikuwa amewapa Mwamba waunywee walipoona kiu, nyoka wa shaba kuwaponya walipokuwa wagonjwa, na hata hivyo, pamoja na hayo yote, iliwabidi kuwa na sheria. Walitaka ujuzi wa ki—kitheolojia, kusudi wapate kitu cha kuzozania, na kuundia dhehebu, na kutengana.

³⁸ Hilo ni jambo tu kama lile lililowapata baba zetu wa Kipentekoste zaidi ya miaka arobaini iliyopita wakati Mungu alipomwita mtu huko California, mnegro, jicho moja lenye makengeza, akampa tukio la ubatizo wa Roho Mtakatifu, kutoka hapo ukaundwa Mtaa wa Azusa, ile Misheni ya kale ya Mtaa wa Azusa, kutoka hapo imetawanyika hata ikaenea kote nchini, kutoka taifa moja ukaenda taifa baada ya taifa, mpaka uamsho wa Kipentekoste ulikuwa ukiwaka kila mahali. Ni baraka jinsi gani Mungu alikuwa ametoa kwa neema!

³⁹ Wengi wao wasingeweza kuandika majina yao wenyewe, baadhi yao walikuja kanisani wamevaa matambara. Walitembea kwenye njia ya reli na kuokota makonzi ya mahindi na kuyatwanga kwenye reli, maskini akina mama, kuwalisha watoto wao kusudi waume zao waweze kuhubiri Injili. Walizungukazunguka, wakadhihakiwa, wakafanyiwa mizaha, na kuitwa watakatifu wanaojifingirisha, wakakaa gerezani usiku kucha. Siku baada ya siku, baadhi yao, walitaka kuwaweka katika hospitali ya wendawazimu, wakasema walikuwa na kichaa.

⁴⁰ Mungu alikuwa amewaandalia mmoja wa miamsho mikubwa sana ambayo taifa hili limewahi kujua. Sijali ilikuwa ni lini, hapajakuwapo na uamsho kama uamsho wa Kipentekoste. Hiyo ni kweli. Wesley kamwe hakuwa nao, hakuna hata mmoja wao aliyekuwa nao, Spurgeon, Calvin, Knox, watengenezaji mashuhuri, bali kamwe hawakuwa na uamsho kama ule uamsho wa Kipentekoste, kitu kikubwa kuliko vyote kilichoipiga dunia tangu Roho Mtakatifu aliposhuka kwenye Siku ya Pentekoste, hakuna kitu. Sasa hivi wa—wamepata wongofu zaidi mwaka uliopita, kanisa lenyewe liliweka maongofu mengi kuliko, karibu, makanisa mengine yote yakiwekwa pamoja. Mlimsikia Billy Graham akinena habari zake si muda mrefu uliopita? Huwezi kulipuuza.

⁴¹ Tulikosea wapi? Kama vile Israeli walivyofanya, tusingeweza kuendelea tu, kwenda jinsi Roho Mtakatifu alivyokuwa akituongoza, ilitubidi kuongeza kitu fulani kusababisha kuingia kwa kutokuamini. Kama Israeli wangiendelea kufuata njia ambayo Bwana alikuwa akiwaongozea, katika majuma mawili wanalikuwa katika nchi ya ahadi, bali iliwabidi kubadilisha kitu fulani.

⁴² Na kama kanisa la Kipentekoste lingeliendelea katika Roho, jinsi Mungu alivyoliagiza kwenda, na tayari alikuwa amethibitisha ya kwamba alikuwa ndani yao, tungekuwa tukiishi katika Utawala wa Miaka Elfu. Lakini walifanya jambo lile lile walilofanya huko nyuma, kama vile Biblia ilivyosema katika Wakorintho. Mambo hayo yalikuwa ni mifano yetu, yaliyowapata hutupata sisi.

⁴³ Ilikuwaje? Jambo la kwanza tusingeweza kuwa, kuendelea kuongozwa na Roho katika kundi la waaminio, ilitubidi kuwa na kitu fulani cha kujibandikia jina, tulitaka kuunda dhehebu. Kwa hiyo walikuwa wameunda, na kile kilicholisababisha mtu fulani alipata ufunuo ya kwamba watu wanapaswa kubatizwa katika Jina la Yesu badala ya Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Na badala ya hayo, basi ilikuwaje? Ilibidi lile Baraza Kuu la kale liwe Assemblies of God basi. Ilikuwaje? Wale wa Jina la Yesu iliwabidi wajiundie dhehebu lililoitwa P. A. ya W., lile P. A. J. C., na yote mbalimbali, mmoja akija juu ya farasi, huyo mwingine akija juu ya wingu.

44 Hapo ndipo mlipokosea, hapo ndipo mnapotenda dhambi mbaya sana. Kwa nini hamkuachana nalo? Kama hilo Jina *Yesu*, na mambo yao yote madogo mliyo nayo, na kadhalika, hayakuwa sahihi, Mungu alisema, “Kila,” ama, *Yesu* alisema, “Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hajaupanda utang’olewa.” Utakuwa bure iwapo si wa Mungu. Na kama ni wa Mungu, ni nani atakayeukomesha? Jambo ndilo hilo. Achana nao. Acha Mungu awe ndiye Mtawala.

45 Lakini ilitubidi kujiundia madhehebu. Sasa tuna Umoja, Uwili, Utatu, na *masalaale*, jamani, tumetengana, tunazozana, makundi madogo, “Sisi ndio kubwa kuliko wote.” “Sisi ndio wachache.” “Sisi ndio wengi.” “Sisi ni *hiki*, sisi ni *kile*.” “Tuna yaliyo bora kuliko yote, tuna pesa nyingi zaidi, tuna wamishenari wengi zaidi, tuna . . .” Loo, jamani! “Hatujagawanyika,” haitupasi kugawanyika, “sisi sote ni Mwili mmoja, mmoja katika tumaini na Fundisho, mmoja katika upendo.” Roho Mtakatifu! “Twendeni mbele askari Wakristo kama vitani,” tukiwa na kitu kimoja mbele yetu, si dhehebu, “bali msalaba wa *Yesu*, ukitangulia.”

46 Daima imekuwa kwamba watu wanataka kungezea sehemu yao, kufanya yale wanayowazia kwamba yanapaswa kufanywa. Jambo lile lile lilitukia wakati Israeli waliwazia walitaka kuwa na mfalme, Mungu alikuwa ndiye Mfalme wao. Mungu daima ametaka kuwa Yote katika Yote kwa watu Wake, bali wanadamu wanataka kujifanyia kitu fulani ndani yake, maana hatuna budi kuwa na wazee wa wilaya, hatuna budi kuwa na ma-Ph.D., nasi hatuna budi kuwa na vyeo hivi vingine vyote vikuu, na kadhalika, kutufanya mtu wa kuangaliwa, ambaye ndugu wengine ambao . . . Mwasema, “Vema, watazozana, na kupigana, na kubishana, na kufanya ujanja wapate jambo la kujivunia,” kama tusemavyo. Mbona, ni fedheha! Inaleta kutokuamini.

47 Biblia ilisema, “Mnawezaje kuwa na imani wakati mnajiona kuwa bora nyinyi kwa nyinyi?” na mambo kama hayo. Mnawezaje kufanya hivyo mnapojaribu kusema, “Mtu wa wilaya yumo humu, hatuna budi kumsikiliza; askofu yumo humu, inatubidi kumsikiliza; mzee wa jimbo yumo humu, inatubidi kumsikiliza”? Ukijaribu kuwa *mtu fulani* katika dhehebu lako, huwezi kufanya hivyo na kisha umwamini Mungu. Huna budi kuachana na kila kitu na kumwamini Mungu. Hapo ndipo Pentekoste ilipoanzia. Hiyo ndiyo Penteko- . . . iliyokufanya wewe Mpentekoste.

48 Neno *kanisa* linamaanisha “walioitwa watoke.” Israeli waliitwa watoke, Pentekoste ilikuwa walioitwa na kutengwa. Israeli ilikuwa ni Kanisa la Mungu, Pentekoste ilikuwa ni Kanisa la Mungu wakati lilipoitwa litoke na kutengwa. Lakini mnafanya nini? Inawabidi kutenda kama hao watu we—wengine, inakubidi kufanya mambo wanayofanya, u—unataka kuwa kama wao.

49 Wakati Israeli walipotaka mfalme, maskini mzee mwema nabii Samweli, aliwaita, naye akasema, “Sikilizeni, nataka kuwaambieni jambo fulani.” Kwa maneno mengine, namna hii: “Hamtaki kuwa kama Wafilisti, msiwe kama mataifa mengine ya ulimwengu, wana wafalme wao, bali ninyi mna Mfalme mmoja, huyo ni Yehova.” Nabii yeyote wa kweli angewaambia hilo, sio kuwaelekeza kwenye kitu kingine, awarudishe kwa Yehova; acheni awaongoze, acheni awaongoze. Vema, walitaka kuwa kama mataifa mengine kwa vyovyote vile, ndipo mzee Samweli akasimama, akasema, “Mungu ndiye Mfalme wenu.”

50 Mungu ndiye Mfalme wetu. Msijaribu kuyaiga mambo ya ulimwengu, mataifa mengine, acheni waendeleo wakitaka. Kama hao watu wengine wanataka maaskofu wao wakubwa, waliovalia nadhifu sana, na wahubiri wasomi sana, na upuuzi huu wote wa Hollywood, acheni wawe nao, bali huo si kwa ajili ya watoto wa Mungu. Roho Mtakatifu ndiye Kiongozi wetu, Ndiye Kiongozi wetu wa kiroho. Huhitaji mambo haya, wao wanayataka, acha wawe nayo, si wewe, hayo hayakufai.

51 Sasa, tunaona kile kilichotukia, Samweli aliwaambia I—Israeli, akasema, “Mungu alinituma niwe nabii wenu. Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia?” Wazia hilo. Naye akasema, “Je, nimewahi kuwaomba pesa zenu? Nimewahi kuchukua pesa kutoka kwenu?”

52 Ndio kwanza nipate barua kutoka kwa ndugu mmoja huko Arizona, ambako kiongozi fulani mashuhuri alikuwa na mkutano. Na katika mkutano huu, kutoka kwenye kanisa dogo, si zaidi ya watu wanaoketi papa hapa, iligharimu kanisa hilo dola elfu sita, mtu *huyu* ni mmojawapo wa hiyo halmashauri, kumwalika mtu huyo, iligharimu elfu kumi kwa matangazo. Na kuliwazia hilo, ndugu, yale dola elfu sita zingefanya katika huduma ya kimishenari, ambapo ninajua mahali ambapo ndugu wanahubiri Injili bila viatu miguuni mwao!

53 Nasi tunaweka mamilioni ya dola katika majengo makubwa mno. Sizungumzi juu ya mtu yeyote yule, ninazungumza juu ya kitu hicho chote kwa jumla. Majengo makubwa, nimeona hivi majuzi tu ambapo shirika kubwa linaweka milioni sita, ninaamini, dola milioni tatu hadi sita katika jengo la ofisi, huku wamishenari wakiwa na njaa hudumani, nasi tunahubiri Yesu yuaja upesi. Ni wapi ambapo unaweza kupata busara katika jambo hilo, enyi watu? Ninaninii tu, nimechanganyikiwa kabisa, silielewi.

54 Maisha yako, kile maisha yako yasemacho, kwa kweli, unayowazia moyoni mwako. Yesu alisema, “Ukisema jambo moja, na kufanya lingine,” alisema, “enyi wanafiki! Unawezaje kunena mambo mema kwa kinywa chako, huku moyo wako unawazia lingine?” Matendo yako yananena kwa sauti kubwa

kuliko maneno yako. Kwa nini tunaamini Yesu anakuja, na kufanya mambo haya? Hatuna wakati kwa ajili ya mambo hayo.

⁵⁵ Samweli alisema, “Sasa, niambieni iwapo niliwahi kusema lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia.”

“La,” wakasema, “kila kitu ulichotwambia kilitimia.”

⁵⁶ “Niambieni wakati nilipowahi kuchukua pesa zenu, niambieni.” Kisha kasema, “Sasa, kama mkianza kutenda kama hao wengine, mnapomleta mfalme humu ndani, na kubadilisha kitu fulani chini ya Yehova...”

⁵⁷ “Vema,” wakasema, “mnaona, huyu atakuwa mfalme wetu, nasi tutakuwa kama watu wengine. Mbona, ita— itafanya kazi vizuri zaidi. Tutakuwa na mtu ambaye tunaweza kumzungumzia, mtu anayeweza kutufariji, mtu atakayekuwa mambo haya mbalimbali kwetu, atakayetujibu.” Loo, ndugu, kama wewe ni wa kiroho tu vya kutosha, Mungu atakujibu.

⁵⁸ Wanajaribu kulikwepa suala lenyewe la kuzaliwa mara ya pili. Hilo ndilo linalotukia. Sasa, watu hawawezi kuwazia juu ya huku kuzaliwa upya, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kadhalika. Ulipataje kuja hapa kuwapo bila kuzaliwa kwa kawaida? Usingeweza kufanya hivyo, hakuna njia hata kidogo kwako kufanya hivyo, kwako kuwepo, na kuweza kutembea huku na huku na kujua, bila ya kuwa na kuzaliwa kwa kawaida. Hiyo ni kweli? Vema, ni jambo lile lile katika kiroho. Kama hujazaliwa mara ya pili, hujui lolote kukuhusu.

⁵⁹ Ungewezaje kumchukua mtu ambaye alikuwa akitaka kuajiri kundi kubwa la watu, akisema, “Nina biashara hapa nje,” mtu anayeenda makaburini, upesi tu awezavyo kukimbia, akikimbia kwenda makaburini?

“Unaenda wapi, bwana?”

“Loo, nina mradi mkubwa mno hapa nje, ninaenda kuwatafuta watu wa kunisaidia.”

“Ati watu wa kufanya *nini*?”

“Kunisaidia.”

“Unaenda wapi?”

⁶⁰ “Makaburini. Loo, niliona majina kote mahali hapo!” Hivyo ndivyo ilivyo, majina tu. Hivyo ndivyo tumekuwa, lundo la majina ya Kipentekoste. Hiyo ni kweli. Tunahitaji kitu kilicho na Uhai ndani yake. Hupati uhai makaburini, katika dhehebu. Ungeweza kuwahubiria usiku kucha na mchana kutwa, hamna kitu hapo cha kusogea.

⁶¹ Kazi yako haitafanyika wakati unapowaambia watu Bwana yuaja, na ku—kufanya uinjilisti, na kwenda mitaani na kushuhudia, na kumfanyia Mungu kitu, unawezaje kufanya hivyo wakati wamekufa? Huna budi kwenda mahali ambapo pana Uhai, mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili. Kanisa halina

budi kuzirudia kanuni za Kristo, kurudi kwenye kuzaliwa upya, kumrudia Roho Mtakatifu, kurudi kwenye mikutano ya maombi ya usiku kucha, mahali panapowaka moto kwa ajili ya Mungu, badala ya *hayo*.

⁶² Unasema, “Vema sasa, mimi ni mfuasi wa *hili*, mimi ni mfuasi wa *lile*.” Je, wewe ni Mkristo? “Naam, mimi ni mfuasi wa *hiki-na-hiki*.” Hicho ni kitu kilichobuniwa na ulimwengu, kadiri kilivyotimiza zamu yake, lakini ninajaribu kutoa hoja sasa, ndugu, tulieni tu kwa dakika moja.

⁶³ Baadhi yenu ninyi ndugu wazuri, washupavu wa kimadhehebu, msianze kujifurukuta na kupiga mayowe, maana ni—ni—ninajua wewe ni ndugu mzuri. Kama vile yule mvulana mdogo alivyokuwa, aliyekuja kula sambusa, naye anakula, ndipo akasema, ya kwamba ma—maskini paka alikuja, na kulialia karibu naye, aliona mkia wake umekaa sakafuni kwa hiyo akamfanyilia tu chini kidogo. Maskini huyo paka akaanza kulia vikali, ndipo mama yake akasema, “Kadogoo, usipoacha kuvuta mkia wa paka huyo, nitatoka na kukupiga kofi mashavuni.”

⁶⁴ Kasema, “Mama, siuvuti mkia wake, nimemfanyilia chini kidogo tu, yeye analia vikali, ndiye anayevuta.” Hiyo ni kweli.

⁶⁵ Sasa, angalieni, loo, kufanyilia Injili chini kidogo tu. Tunachotaka kufanya ni kuiweka mahali pake. Basi kanisa lilifanya kosa lake baya sana wakati lilipounda dhehebu lake la kwanza. Mlifanya nini? Mnasema, “Vema, wa—walianza kuleta hoja.” Vema, kama ulikuwa ni mwaminio wa kweli wa Mungu, Mungu ametuahidi kwamba kama Yeye hakuupanda, kamwe hautaenda popote, kwa vyovyote vile, achana nao, utafikia mwisho wake. “Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hajaupanda utang’olewa.” Hiyo ni kweli kabisa. Lakini iliwabidi tu kufanya hivyo.

⁶⁶ Sasa, tunaona baada ya baraka zote kuja kwa Israeli, hata hivyo walitaka, Kutoka 19, walitaka kuwa na—walitaka kuwa na sheria. Walitaka kuwa na kitu ambacho wangeweza kufanya wenyewe, baadhi ya siku za Sabato ambazo wangeweza kuadhimisha, ama baadhi ya maagizo ambayo wangeweza kutekeleza, ama—ama *kitu kingine* kilichokuwa ndani, walicholetewa ambacho wangeweza kufanya wenyewe. Na kama unaweza kufanya jambo moja kujiokoa, basi hakuna chembe yake moja ambayo ni neema. Sheria ni kile unachofanya kuhusu neema ambayo Mungu amekuonyesha kwa kukuokoa.

⁶⁷ Kama vile nimesema mara nyingi, sitembei na wanawake wengine kwa sababu nahofia mke wangu atanitaliki, sizururi na wanawake wengine kwa sababu nampenda mke wangu. Jambo ndilo hilo. Siamini kwamba unapaswa kuzurura. Lakini sheria siyo inayoidumisha, nadhiri yangu ya ndoa, ni upendo wangu.

⁶⁸ Na ni, sababu ya mimi kumpenda Mungu, si kwa sababu ninahofia angenipeleka kuzimuni, siamini angefanya hivyo, lakini kwa sababu ninampenda sana, sitaki kufanya hivyo. Hakuna kitu ndani yangu cha kunifanya nifanye hivyo, ninampenda kupita kiasi, nisingemduru kwa chochote. Bila shaka, ninampenda.

⁶⁹ Na wakati wanaume na wanawake wanapofikia mahali, “Vema, kweli ninapaswa kukaa nyumbani na kuangalia mchezo huu mzuri usiku wa leo, na lakini ni—nitawaambia, watafikiri nimerudi nyuma nisiposhuka kwenda kanisani.” Halafu unaketi mle na kulala kwa vyovyote vile, afadhali ungalikaa nyumbani, na kuangalia kitu ambacho ungefurahia zaidi. Lakini furaha yako inapokuwa ni Bwana, naye Bwana ndiye furaha yako, huwezi kukosa kwenda kanisani, basi unafika mahali fulani.

⁷⁰ Kanisa lilikuwa katika hali nzuri zaidi miaka arobaini iliyopita kwa ajili ya Kuja kwa Bwana Yesu, kuliko lilivyo usiku wa leo, bora zaidi. Walikuwa karibu zaidi na Mungu, walikuwa na Mungu zaidi miongoni mwao, walikuwa na Roho zaidi miongoni mwao kuliko walivyo naye usiku wa leo.

⁷¹ Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Kwa sababu tulijitenga, kila kundi dogo peke yake, likienda huko nje na kuliambia hilo li—lingine, “Vema, maskini banda lile la mwewe pale, hili *ndilo*. Pale, *hawanalo, tunalo* sisi.” Na tofauti zenu ndogondogo za mafundisho na kadhalika, wala Mungu asingezingatia jambo hilo kiasi hicho. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.]

⁷² Kama hatuna upendo, inaleta faida gani kwa vyovyote vile? “Nijapojua siri zote, na kuzifahamu siri zote za Mungu, nijapokuwa na imani ya kuhamisha milima, na kutoa ninii yangu, mali yangu yote kwa maskini, na mwili wangu uhomwe moto kama dhabihu, wala sina upendo, si kitu mimi,” alisema Paulo, Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 13.

⁷³ Mnaona, m—mnakosa jambo kenyewe mnapoanza kujitenga, inaonekana hamna imani, mnapoanza kujitenga wenyewe, “Sisi ni kundi *hili*, sisi ni wafuasi wa *hili*, hatuna uhusiano wowote nao.” Na yote ni Roho Mtakatifu. Kila moja ya makundi hayo yote yananena kwa lugha, kila moja ya makundi hayo lina wema na wabaya miongoni mwao, kama tu vile kundi la kwanza lilivyokuwa nao, nao daima watafanya hivyo. Naye Mungu huwapa Roho Mtakatifu hao wanaomtii. Kwa hiyo ni nani waliomtii? Wale waliomwamini na kulikubali, hao ndio waliomtii.

⁷⁴ Mnaona, lakini hatuna budi kuwa na kitu cha kufanya ndani yake sisi wenyewe, tunataka kuwa kama Wamethodisti, kama Presbiteri, Baptisti, Katoliki. Hatuna budi kuunda dhehebu. Tuna . . . Hilo ndilo jambo lile lile aliloshindiwa Martin Luther, si Martin Luther, yeye hakulianzisha, John Wesley hakulianzisha, kundi lilolowafuata ndilo lililolianzisha. Hiyo

ni kweli. Hawakulianzisha, la, bwana, walilidumisha safi, lakini walipoondoka, ndipo awamu yao ya pili ikaanza kuunda dhehebu.

⁷⁵ Na hivyo ndivyo tu ilivyokuwa huko nyuma mwanzoni. Kundi la kwanza lilitambua ilikuwa ni Mungu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao wakadumu nalo, lakini kundi la pili lilipokuja, “Vema, hatuna budi kufanya *hivi*, hatuna budi kujitenga nao, inaonekana hawana imani, nasi *tunayo*. Nasi tutalifanya kundi letu hapa lijiondoe.” Ndipo basi hilo likamfanya kiongozi fulani aende *huku*, na kumvuta *huyu*, na *huyu* akivuta *huku*, *huku*; mnaona, jambo lile lile hasa walilofanya Israeli.

⁷⁶ Walitaka, Kutoka 19, walitaka sheria, walitaka jambo fulani wangeweza kufanya wenyewe, iliwabidi kuwa na kitu cha kufanya ndani yake. Iliwabidi kuwapandisha jamaa vyeo, iliwabidi kuwa na kazi ambazo wangeweza kufanya wenyewe.

⁷⁷ Mungu ataleta kazi. Kama utatembea tu katika neema, utafanya kazi kuliko unavyofanya sasa hivi na Shirika la Msaada la kina Mama, na upuuzi huu mwingine wote ambao umeongezwa kanisani. Supu ya jioni ya kumlipa mhubiri, mlipata wapi kitu kama andiko hilo? Zaka humlipa mhubiri, yeye anapaswa kuishi kwa zaka za watu. Lakini ilitubidi kupata kitu kingine cha kufanya, hatuna budi kuwa na sehemu yetu ndani yake. Na kama ninii, hawawezi kufaulu, kuna shirika lingine litakalofanya hivyo, shirika lingine.

⁷⁸ Njia ya Mungu ni sawa. Zaka na matoleo huenda kwa Lawi, ambaye alikuwa mhudumu. Kama kila mtu angelipa zaka zao, isingewabidi kuwa na supu yoyote ya jioni. Mnaona, mlichukua kitu kingine, na kuacha kutoa zaka. Mnasema ni hoja ya Agano la Kale. Ningetaka mnithibitishie. Hiyo ni kweli. Hamwezi kufanya hivyo kwa Neno la Mungu, ni utaratibu wa Agano Jipya, pia. Mungu hufanya utaratibu mmoja, kamwe hauwezi kubadilishwa, hauna budi kubaki hivyo.

⁷⁹ Kama vile Damu, mtu fulani anasema, “Vema, sisi—sisi, nawaambia, tu—tunafanya *hivi* na kufanya *vile*, nasi tuna kanuni za imani, na tunajaribu kuwaleta watu kwa Kristo kwa kuwaelimisha, tunajaribu kuwaleta kwa Kristo kwa kuwaundia dhehebu,” tunapigana tu na upepo, haifai kitu, kuna njia moja tu ya kumwenda Kristo, hiyo ni kupitia kwa Damu. Huo ndio mpango wa Mungu kwanza kabisa, Naye hawezi kubadilisha, tunakuja kupitia Kristo kwa njia ya Damu. Na baada ya kuipokea ile Damu sisi, ile kemia ya Damu kuziondoa dhambi zetu, na kutusafisha na uovu wetu, ndipo tunampokea Roho aliye katika Damu, ambaye ni Roho Mtakatifu ambaye anaturudia, na kutufanya wana na binti za Mungu, hiyo ni kweli, ndipo ninyi ni viumbe vipya katika Kristo, ndipo mna tukio lile lile walilokuwa

nalo hapo mwanzo. Mnaishi maisha ya namna ile ile, na kufanya kazi za aina ile ile walizofanya hapo mwanzo.

⁸⁰ Naam, Kutoka 19, ndipo Biblia ikasema ni safari ya siku kumi na moja kutoka Mlima Sinai hadi Kadeshi. Siku kumi na moja baada ya wao kushindiliwa theolojia, kazi zao walizotaka kufanya, walifanya kosa kubwa kuliko yote waliyowahi kufanya. Huko Kadeshi ndiko walikolitilia shaka Neno la Mungu. Tangu wakati walipokuwa wakifuatana na Mungu, mpaka waliposhindiliwa, na ndipo walipofanya hivyo walifanya kosa lao baya sana, kuamini ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ni kweli.

⁸¹ Walichukua madhehebu yao, yale makabila kumi na mawili mbalimbali yakatuma mwakilishi kwenda huko na kuipeleleza nchi. Wawili kati yao walienda kule na kuleta ushahidi, walileta ushahidi mmoja kwamba ilikuwa ni nchi nzuri. Yoshua na Kalebu walibeba kichala hiki cha zabibu, labda, begani mwao, kila mtu akaonja, akasema, “*Hmm*, jamani! Ni nzuri sana, ni nzuri sana.”

⁸² Lakini waliporudi mbele ya kusanyiko, walisema, “Upinzani ni mkubwa sana, kamwe hatuwezi, hakuna haja ya sisi kujaribu. Mbona, tunaonekana kama panzi kando ya hao majitu wakubwa wa elimu huko nje, hao maaskofu wakuu, na madaktari wa uungu. Kuna jambo moja tu, maskini miaka yetu mi—miwili ya shule ingewezaje, elimu yetu ndogo ya msingi ingelinganishwaje na Daktari, Ph.D., L. maradufu D., S.Q.U.T., hizi zingine zote? Tungewezaje kufanya hivyo na hawa jamaa wakubwa mno?” Hilo silo. Mungu aliahidi ile nchi, elimu haina uhusiano wowote nayo.

⁸³ Mungu aliahidi Roho Mtakatifu kwa yeyote atakaye, na aje. Hupambanui kati ya maharagwe yaliyopasuliwa na kahawa, inaleta tofauti gani? Kama huwezi kukariri ABC zako, inaleta tofauti gani, mradi tu umepata tukio?

⁸⁴ Wakati Petro na Yakobo waliponyakuliwa, ama, Yohana, kwenye lango Zuri, ambapo walikuwa wamemfanya mtu aliyekuwa kiwete kutembea, wakamfanya atembea, aliyekuwa kiwete tangu tumboni mama yake, Biblia ilisema walikuwa watu wasio na elimu wala maarifa, bali hata hivyo walitambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Hizo ndizo sifa za Mpentekoste halisi, si kwamba una digrii ngapi, umechukua digrii kiasi gani, Shahada ya Sanaa, ama kama wewe ni Ph.D., ama LL.D., ama chochote kile, hizo hazina uhusiano wowote nalo, ni kuwafanya watu wajue ya kwamba umekuwa pamoja na Yesu Kristo, kuwaacha watu wajue ya kwamba kuna *Kitu fulani* huko nyuma ambacho kimeichochea nafsi yako, hiyo ndiyo Pentekoste.

⁸⁵ Wakati mwingine ninaona jinsi kanisa linavyopata... Niliacha kanisa la Kibaptisti nipate kuwa Mpentekoste,

nililiacha kwa sababu nilijua walikuwa na kitu fulani, lakini nilipofika hapa, limejiundia madhehebu kwa dhati kama Baptisti ilivyokuwa, wabaya zaidi. Hiyo ni kweli.

⁸⁶ Sasa, tunatoka nje na kuangalia, na kuangalia kote, na kuona safari ya siku kumi na moja kutoka kwenye theolojia hadi kutokuamini kabisa, tangu siku walipopata torati mpaka hatimaye walipoingia katika kutokuamini kabisa. Hawa hapa wawili wanarudi waliokuwa na ushahidi.

⁸⁷ Kanisa la Kipentekoste, miaka arobaini iliyopita, lilileta ushahidi mmoja mzuri kwamba kulikuwako na Nchi ng'ambo ya hapo, kwa sababu walikuwa na ushahidi wa kunena kwa lugha. Lakini ndugu, huo sio ushahidi pekee, si kwamba tu ilikuwa na zabibu nzuri mle, bali ilikuwa na maziwa na asali ikitiririka, ilikuwa na kila kitu. Lakini waliridhika tu na hizo zabibu, na kusema, "Hiyo ni, nadhani hivyo tu ndivyo ilivyo." Hivyo ndivyo kanisa la Kipentekoste limefanya, "Matendo 2:4, Matendo 2:4, Matendo 2:4," mpaka mkapata zabibu nyingi sana, naamini zilitoka kwenye zabibu halisi zikafikia zabibu kifaurongo, zabibu kali. "Matendo 2:4, Matendo 2:4," mpaka karibu mnakuwa wahubiri wa 2 kwa 4, hiyo ni kweli, kunyonya kwenye dhehebu. Huh!

⁸⁸ Jambo moja, hawanilipi, niko huru kuihubiri Biblia. Na mradi tu Mungu ananijalia kuishi, nitasimama papo hapo kama shahidi dhidi ya uovu. Sijali ni wapi... Hakuna kitu kibaya kuhusu dhehebu, dhehebu ni sawa. Torati ilikuwa sawa, ilitimiza kusudi lake, hiyo ni kweli, lakini torati haikuwafaa kitu, haikuwapa neema yoyote. Torati haikuwapeleka kwenye nchi ya ahadi, la, bwana, torati ilikoma, Yoshua akawavusha, naye Musa, mtoa sheria, akafa.

⁸⁹ Na vivyo hivyo kanisa la kimadhehebu litakufa, ndipo neema, na nguvu za Mungu, na Roho Mtakatifu atarudi Kanisani kulinyakua Kanisa liingie kwenye Nchi ya Ahadi. Naam, ilitimiza kusudi lake, bali haikuwa kitu ambacho Mungu alikuwa anataka. Torati ilikufa, ikakoma kuwepo, Musa, yule mtoa sheria, akafa; Yoshua, yule aliyeamini ile ahadi, akaendelea mbele, mbele.

⁹⁰ Sasa angalieni, wote walisema, "Loo, hatuwezi. Itafanya nini? Itaharibu urithi wetu." Hivyo ndivyo ninyi Wamethodisti mliyowazia, hivyo ndivyo ninyi Wabaptisti mliyowazia mlipoenda kwenye mpaka huo na kuangalia huko, kasema, "Loo, si—siwezi kufanya hivyo, na—nawaambia, wakifanya hivyo, wataninii, dhehebu langu la Methodisti litanifukuza." "Dhehebu langu la Baptisti litanifukuza." "Presbiteri yangu, itanifukuza." "Kama nikianza kunena kwa lugha, na kusimama kwenye mimbara yangu, kisha mtu fulani katika kusanyiko langu aanze kunena kwa lugha, nisipowakataza, mbona, watanifukuza kwenye madhehebu." Haya basi, jambo lile lile.

⁹¹ Hebu niwaambie matokeo ya hilo, fungueni Waebrania mlango wa 6, na Waebrania mlango wa 10, linganisheni vifungu hivyo pamoja, “Kwa maana sisi tuliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kuonja nguvu za Ulimwengu ujao;” mnaona, “wale walioupokea ujuzi wa ile kweli, kisha wakageuka; kuanguka hata toba; kwa kuwa wamejisulubisha tena kwa Mwana wa Mungu, na kumfedhehi kwa dhahiri.”

⁹² Hili hapa: Mtu ameitwa kuwa mhubiri, naam, bwana, “Bwana aliniita.” Sawa. Vema, anakuja na kutubia dhambi zake, amehesabiwa haki, anakuwa mwaminio mzuri. Sasa, jambo lingine analofanya, angali anavuta sigara, angali ana tamaa mbaya, anawaangalia watu wa kilimwengu, wanawake wa kilimwengu, naye, tamaa mbaya na kadhalika zimo moyoni mwake, anajua hilo si sawa, hilo halimfai mhubiri, kwa hiyo anashuka na kumwomba Mungu amtakase. Yuko kwenye hatua ya pili basi, “Ondoa kitu hicho kutoka kwangu.” Sasa, anaangalia kwenye Nchi ya Ahadi, mkwamia mpakani, anafikia mahali ambapo hawezi kwenda mbele zaidi, hana budi kuvuka Yordani, hivyo tu, ama abaki nyuma. Mnaona? “Walikuwa washiriki, wakapewa nuru, na kupokea maarifa ya ile kweli.” Naye Kristo ndiye Kweli.

⁹³ Tunaingiaje ndani ya Kristo? Kwa shirika? Kwa kupeana mikono? Kwa dhehebu? Kwa ubatizo wa maji? La, bwana. “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri, Walutheri, wa Umoja, Uwili, Utano, chochote ulicho, kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili huo.

⁹⁴ Lakini, mara tu, amepokea maarifa, anakuja pale na kuangalia, akasema, “Naam, loo, hilo ni zuri sana, bali kama nikipokea hilo, dhehebu langu litanifukuza. Siwezi kufanya hivyo, kwa sababu hawaliadini. Siwezi kuwaacha watu wangu wafanye hivyo. Kama nikifundisha hayo kanisani mwangu, watakuwa na nini? Watawatuma wazee wa wilaya waje pamoja, watawatuma watu mashuhuri waje, waseme, ‘Ukifanya hivyo, ukiruhusu hilo, huyo utaondolewa kwenye hili dhehebu. Kama una *fulani-wa-fulani* hapa, tutakufukuza tu kwenye ushirika.”

⁹⁵ Ee Mungu! Kwa mhubiri asiye na msimamo kama huyo, anahitaji kurudi Kalvari. Ana kasoro, unaposhawishika ya kwamba ni Neno la Mungu, wala huna imani halisi ya kutosha ya Roho Mtakatifu kutetea yaliyo kweli. Haleluya!

⁹⁶ Mwanamume atamheshimu mwanamke, huenda akawa mweusi kama makaa, bali anamwona mwanamke huyo kama mwanamke, yeye anatetea heshima ambayo ni mali ya mwanamke, mwanamume halisi atamvulia kofia, kweli, maana anatetea kilicho sahihi katika kanuni. Hiyo ni kweli kabisa. Huenda akawa na sura mbaya kama toka-nje wote,

atakuwa na heshima mara elfu moja zaidi kwake kuliko vile angekuwa nayo kwa mmoja wa hawa malkia wa Hollywood, ama chochote kile, kama ana *uwanaume* halisi kwake. Kweli.

⁹⁷ Vivyo hivyo na Mungu anapompata mtu ambaye angeweza kuweka tumaini la kutosha ndani yake kumfunulia Neno Lake, naye atasimama, asimame juu ya imani ya Biblia, na kusema, “Nithibitishieni.” Hiyo ni kweli. Ndipo unachukua Neno la Mungu, kila Neno jinsi tu lilivyoandikwa, na kulihubiri jinsi tu lilivyoandikwa, Mungu anawajibika kuja moja kwa moja nyuma pale akilithibitisha kwa ishara na maajabu yanayofuata, kama alivyosema angefanya.

⁹⁸ Si kusimama kwenye ushahidi mmoja, kuna ushahidi zaidi, kuna nyumba, kuna mahali, kuna mabustani, maziwa, na asali, na vyakula vizuri, na vitu vingi, maji yanayotiririka kutoka milimani. Kila kitu ni kizuri kule, sio kichala kimoja tu cha zabibu, bali hapo ndipo tunaposimamia, “Mungu abarikiwe, nimepata Roho Mtakatifu, ushahidi wa kunena kwa lugha.” Hiyo ni sawa, inaonyesha mtu fulani alienda kule. Lakini kwa nini unasimama kwenye mpaka huu?

⁹⁹ Mnaona, “Walifanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kuonja nguvu za ulimwengu ujao,” kuona ya kwamba watarudi katika mtindo ule ule wa kale ambao Wamethodisti walirudia, Wabaptisti walirudia, Wapresbiteri walirudia, “na kumsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.”

¹⁰⁰ Nasi tunaona katika Wakati wa Kanisa la Laodikia kwamba Yeye alikuwa nje ya kanisa la Kipentekoste akijaribu kurudi ndani. “Kumfedhehi hadharani.” Loo, Mungu aturehemu, ndugu. Kama msipokubaliana nami juu ya mambo haya, yachunguzeni Maandiko. Tafuteni kujua siku tunayoishi, angalieni mahali ilipo.

¹⁰¹ Nina mawaidha, sitayasoma sasa, lakini haya *hapa*, Demos Shakarian anayafanya yaandikwe, na mtu, mtu wa Hollywood, aliyekuja kunisalimia kwa mkono, halafu akaanza kuzungumza Kifaransa, naye mkalimani wa UN pale akatoa tafsiri, pamoja na mwanamke Mfaransa, kasema, “Kwa sababu umechagua njia ngumu, lakini hiyo ni NJIA YANGU, usiogope yale watu wasemayo kukuhusu, kwa kuwa niko pamoja nawe, nami nitakuwa pamoja nawe, nami nitatimiza mambo mengi na kwa wingi sana.”

¹⁰² Nimeyaandika papa hapa, na yakatiwa sahihi na... Na—na Ndugu Demos Shakarian anayafanya yaandikwe na mthibitishaji rasmi. Naye mtu huyo, Mbaptisti, hakujua lolote kulihusu, bali nilikuwa nikijaribu kusimama pale na kulaani hicho kitu kinachoyapofusha macho ya Wapentekoste, Hollywood kuingia makanisani, uinjilisti wa Hollywood.

¹⁰³ Jamaa fulani atasambaza bahasha, na kusema, “Weka dola ishirini na tano ndani yake, nami nitakuombea,” nakwambia mazao yako yataharibika kama hutafanya . . . acha . . . usipoweka *kiasi fulani* kwenye matoleo. Ilitokea lini ya kwamba Pentekoste inafuata pesa? Mbona, ndugu, katika wakati wa Biblia waliuza walichokuwa nacho na kuligawia kanisa. Siku hizi hatuna budi kuwa na kundi la Makadilaki la sivyo ninyi si wa kiroho. Ni dhambi, ni fedheha.

¹⁰⁴ Tunajaribu kuona kama hatuwezi kujenga kanisa bora kuliko—kuliko walilo nalo *kule*, Mpresbiteri kanisa bora kuliko la Methodist, na kusema Yesu yuaja hivi karibuni. Wanakucheka moja kwa moja usoni mwako. Hiyo ni kweli. Tunachohitaji leo hii si kanisa bora, mngekuwa afadhali zaidi kama mngekuwa na misheni, mngekuwa bora zaidi mkisimama chini ya mmoja wa hii mialoni hapa nje, ama misonobari, bila mahali pa kulaza vichwa vyetu, na kuhubiri Injili, kuliko kupatana.

¹⁰⁵ Tuko katika hali mbaya sana, kanisa lenyewe. Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Kwa sababu tulijitenga, mmoja akajitenga akaenda kwenye *hili*, mmoja akajitenga akaenda kwenye *lile*, tukawa na mawazo makubwa ya kimadhehebu, na kila kitu. Ikiwaonyesha tu hasa, katika mfano, kile walichofanya wakati huo. Nasi tungalisonga mbele na kuingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu.

¹⁰⁶ Ninaamini ya kwamba wakati wa Kuja kwa Yesu Kristo umepita, ninaweza kulithibitisha kwa Biblia, Biblia ilisema, Yesu Kristo alisema Mwenyewe, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” naye Mungu alikuwa mvumilivu, hataki mtu yeyote apotee, alikuwa mvumilivu, akingojea, akingojea, akiizuia ghadhabu, akingojea, aone kama mtu mwingine asingeweza, akingojea, akingojea, akingojea, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mungu ni mvumilivu, akingojea kuliweka Kanisa Lake katika hali ifaayo.

¹⁰⁷ Ni kitu gani? Ni kitu gani? Badala ya kuwa katika hali ifaayo, tunaenda mbali zaidi wakati wote. Tunapaswa tuwe tumekuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu, tunapaswa kuwa tumekuwa tukimfanyia Mungu jambo fulani, tunapaswa kuwa tuliingia miaka arobaini iliyopita, lakini la, tungefanya kosa lile lile walilofanya. Walifika Kadeshi, miaka arobaini, ndipo Mungu akawafukuza kwa sababu ya kutokuamini. Ilikuwa ni kitu gani? Shirika. Watu walikuwa wakiangalia . . . Ingetukia nini?

¹⁰⁸ Sasa, mnasema, “Shirika gani?” Ninyi nyote! Jitengeni. Unasema, “Je, ninaweza kuwa Assembly na niwe wa kiroho?” Hakika. “Je, ninaweza kuwa wa Umoja na niwe wa kiroho?” Hakika. Mungu hukupa Roho Mtakatifu kama wewe ni Mkatoliki. Haijalishi wewe ni nini, mradi tu wewe ni mtoto wa

Mungu kwa kuzaliwa katika Roho Mtakatifu, wewe ni mtoto wa Mungu.

¹⁰⁹ Basi usininii tu, kumbuka, ndugu huyo mwingine anavuta apate kujifunika, pia, hiyo blanketi ni kubwa vya kutosha kwenu nyote wawili, Mungu aliifanya hivyo, usiinyakue yote, na kujifunika nayo, useme, “Ganda hata ufe.” Kama unahisi baridi, hebu nikusaidie. Inapofikia mahali hutaki kumsaidia ndugu aliyeanguka! Kama unafikiri ameanguka, msaidie kwa njia fulani, simama katikati ya hayo mapengo, ziba hilo *pengo* kwa upendo. Hiyo ndiyo saruji inayoliunganisha Kanisa la Mungu pamoja, ndiyo saruji ya upendo mtakatifu wa Mungu miongoni mwa ndugu.

¹¹⁰ “Hivi watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu,” ati wakati wewe ni wa Assemblies? “Watu wote watajua ninyi ni wanafunzi Wangu,” kwa nini? Ati kwa sababu ninyi ni wa Umoja? Kwa sababu ninyi ni wa Church of God?

¹¹¹ “Hivi watu wote watajua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninyi kwa ninyi.” Hapo ndipo watakapojua, hapo ndipo ulimwengu utakapojua ya kwamba sisi ni Wakristo, hapo ndipo ulimwengu utakapojua ya kwamba sisi ni ndugu na dada, tunapokuwa na upendo sisi kwa sisi. Hiyo ndiyo alama ya Ukristo, ni kupendana. Tutakapoupata huo, ndipo Mungu atakapoanza kutenda kazi miongoni mwetu na kutuletea maziwa, asali, mambo makuu. Mbona, ni vizuri tunapoona mpango wa Mungu, na kuingia ndani yake.

¹¹² Sasa, tunaona ya kwamba, walifanya nini, mwaminio mkwamia mpakani? “Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika, na, wa Roho Mtakatifu, na kuonja habari za Ulimwengu ujao, na—na wakawa na ujuzi wa ile kweli, wakapokea ujuzi wa ile kweli,” wakatembea na kuiangalia ile Nchi na kusema, “Vema, kamwe siwezi kufanya hivyo,” wakarudi... Hivyo ndivyo hasa hao jamaa wakwamia mpakani walivyofanya siku hiyo. Walifanya nini? Wao, kila mmoja, waliangamia nyikani.

¹¹³ Tunapowazia kwamba Mungu anawajibika kwetu kwa sababu “Sisi ni *hiki-na-hiki*, Mmethodisti hana uhusiano wowote nacho, Mbaptisti hana uhusiano wowote nacho, wa Umoja hana uhusiano wowote nacho, wa Assemblies hana uhusiano wowote nacho,” basi tumekosea. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹¹⁴ Usiyaangalie madhehebu yako, angalia jinsi Roho anavyoongoza, kama Roho anakuongoza, kamwe hatakuongoza kinyume na Neno, kamwe hatatenda isivyostahili, mradi anadumu katika Neno hilo.

¹¹⁵ Mungu alifanya nini? Aliwaacha huko kwa muda wa miaka arobaini nyikani. Hivyo ndivyo hasa alivyowafanyia Wapentekoste. Tulikuwa na ushahidi wa kwanza, kunena kwa

lugha. Loo, mnasema, “Tumekuwa na uponyaji wa Kiungu.” Walikuwa nao, pia, walikuwa na nyoka wa shaba; walikuwa na Mwamba uliopigwa, loo, hakika. “Loo, Ndugu Branham, hebu nikwambie, sisi wa Umoja, sisi Waassemblies, sisi akina *Nanii*, tumepaza sauti, tulicheza katika Roho.” Loo hakika, walifanya hivyo, pia, bali walikaa nje ya nchi ya ahadi miaka arobaini.

116 Uliwahi kuwazia yale waliyofanya? Loo, Mungu aliwabariki, sivyo? Alisema aliwabariki. Walikuza mazao mazuri, walikuwa na familia nzuri, walikaa kule, nao walibarikiwa, na kufanikiwa. Mbona, baadhi yetu sisi Wapentekoste tunaninii, jamani, baadhi yao, mbona, tuna thamani ya mamilioni ya dola, wengi wao. Hakika, sisi. . . Mungu ametufanikisha.

117 Nilisimama si muda mrefu uliopita m—mkutanoni, ndugu aliyeketi hapa sasa, alikuwako, Ndugu Fred Sothmann, nilipokuwa nikizungumza usiku mmoja huko Kingston, Jamaika, huku nikiwa na Wafanyabiashara wa Full Gospel, watu wale wale ninaowatumia kujipenyeza nikijaribu kuuleta Ujumbe wangu kwa watu, kuonyesha ya kwamba kupitia shirika hili la wafanyabiashara. . . Mbona, basi wafanyabiashara wa kanisa wanakuja kwenye mkutano huo, italeta. . . vema, mchungaji asipokuja, kwa namna fulani inamwaibisha. Kwa hiyo kwa njia hiyo ninaweza kufanya kazi mle ndani kujaribu kuupeleka Ujumbe wa Bwana kwa watu ninaowaona, ndugu zangu, ndugu zangu.

118 Ndipo ikawaje? Ni—nilikuwa kwa namna fulani nimehubiri vikali kulipinga. Ndipo kiongozi fulani huyu akasimama, akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “Nitakwambia. . .”

119 Nikasema, “Mna shida gani ninyi wafanyabiashara? Mnafanya nini? Ninyi, kwenye mkutano huo wa biashara usiku wa leo, kila kitu mlichowashuhudia hao Wajamaika kilikuwa, ‘Nilikuwa na biashara ndogo pembeni, haikuwa ikifanikiwa hata kidogo, haleluya, nikampokea Roho Mtakatifu, Mungu akanipa kundi la Wakatoliki, ama, tofau-. . . , ama, Makadilaki, na—na magari makubwa mno, na *hiki* kikubwa mno, Naye akanipa makazi mapya, akanipa *haya* yote.’ Hao watu wana vitu hivyo, hawataki kusikia hayo. Hayo ni kinyume na Pentekoste, Wapentekoste, waliuza kila kitu walichokuwa nacho, wakavigawanya miongoni mwa maskini, nao wakatoka bila kitu. Walitoka pamoja na Yesu pekee.” Hiyo ni kweli.

120 Kiongozi huyu usiku huo, alisimama, akasema, “Lakini Ndugu Branham, nataka kukwambia jambo fulani sasa hivi,” akasema, “hapo ndipo Wapentekoste, kundi hilo la watu lilipofanya kosa lao kubwa zaidi walilowahi kufanya, hapo walipouza nyumba zao, kisha wakawapa maskini.” Simwombi mtu yeyote uuze nyumba yako, ninakuomba tu umfuate Kristo. Lakini ninawaambia, ninanukuu tu Maandiko. Ndipo akasema, “Vema. . .”

Nikasema, “Vema, Ndugu, waliongozwa na Roho Mtakatifu.”

Kasema, “Vema, walifanya kosa.”

Nikasema, “Unataka kuniambia kwamba Roho Mtakatifu angemwongoza mtu makosani?”

Akasema, “Ilihithitisha jambo hilo, ninaweza kukuthibitishia kwa Maandiko.”

Nikasema, “Simama kwa miguu yako na ufanye hivyo, Ndugu.” Nikasema, “Sasa . . .”

¹²¹ Akasema, “Haya basi: Mara mateso yalipoanza dhidi ya Kanisa watu hao hawakuwa na mahali pa kwenda, tayari wameuza nyumba zao na kuwapa maskini, walizunguka-zunguka tu.”

¹²² Nikasema, “Kile hasa Mungu alichowataka wafanye, ndipo Ujumbe ukasambazwa kote nchini. Kama wanalikuwa na nyumba, wanalirudia, lakini hawakuwa na mahali pa kwenda, kwa hiyo walizunguka-zunguka na kuusambaza Ujumbe.” Hivyo ndivyo hasa Mungu alivyowataka wafanye. Watu hawataki kuchukua barabara hiyo tena, hawataki hiyo, loo, la, bwana.

¹²³ Loo, sisi Wamarekani ni wenye manyoya na wanene, nasi tu—tunasogelea tu chini, na hata haitubidi kuketi na kulisikiliza, tunaamka tu na kwenda nyumbani. Hakika, hiyo ni kweli. Hawalitaki.

¹²⁴ Jambo ni kwamba, mnakumbuka ni nani atakayetiwa muhuri na Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, mnajua yale Biblia ilisema? “Wale wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini,” Ezekieli mlango wa 9.

¹²⁵ Ingawa, ninataka kuwaulizeni baadhi yenu ninyi watu: Unaweza kuinua vidole vingapi, usiku wa leo, vya mtu yeyote katika mji huu, ama mji wako unakotoka, anayeugua na kulia, mchana na usiku, kwa ajili ya machukizo ya mji? Inueni mikono yenu. Niambieni, kwamba, “Ninaweza kukuonyesha watu watano katika mji wangu. Ninaweza kukuonyesha watu wawili.” Ama, “Naweza, nikuonyeshe mtu mmoja.” Kama huwezi, weka mikono yako chini. Hakuna mkono ulioinuliwa. Haya basi. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mnaona ninalomaanisha? Tumepoteza ile bidii. Ka—kanisa la Kipentekoste halina budi kurudia hali yake ya asili.

¹²⁶ Tumefanya nini? Tumenenepa tu, na kuota manyoya, na kuketi chini, na kuachilia tu mambo, kuvalia kama ulimwengu, kutenda kama walimwengu, kwenda kwenye burudani za kilimwengu, kufanya mambo ambayo ulimwengu ulifanya, tukiwa na mashirika yetu, madhehebu, na kushindana nayo, na majengo yetu ya kanisa, na kila kitu, kuhubiri, “Loo, naam,

haleluya!” Kama vile David duPlessis alivyosema wakati mmoja, “Hao ni wajukuu, hao si wana wa Mungu, wala Mungu hana wajukuu wowote.” Mungu si *Babu*, Yeye ni *Baba*. Kweli.

¹²⁷ Nasi tunafanya nini? Tunawaleta watoto wetu, tunawaweka kwenye orodha rasmi, na mwenye dhambi huko nje, naye anajiunga na kanisa la Kipentekoste, nasi tunasema, “Loo, hilo si ni zuri sana? Amekuwa Mpentekoste.” Mjukuu.

¹²⁸ Mwana halisi wa Mungu anawaka moto, hachezi, anasimama pale pasipo kujua chochote ila Kristo, Naye amesulubiwa. Hakuna kitu kinachomshikilia ila Mungu, anaongozwa na Roho, hakuna kitu kingine kinachomsumbua. Yeye humfuata Roho popote aendapo. Wenye uhai, kama vile katika Kitabu cha Ezekieli ambapo magurudumu yalienda, mbona, wale Wenye uhai waliyafuata, sasa, angalieni, wale Wenye uhai, si waliokufa, wale Wenye uhai.

¹²⁹ Angalieni kwa dakika moja tu, walikaa pale, wakaoa wake, wakalea watoto, walikuwa na mazao mazuri, walibarikiwa, naam, na—nao walikuwa na wakati mzuri sana. Walikuwa mle ndani. . . Walikaa mle muda gani? Biblia ilisema mpaka wale wapiganaji wote wa kale walipokufa. Hiyo ni kweli. Wale wote waliosema, “Utukufu kwa Mungu, sisi ni Assemblies.” “Vema, utukufu kwa Mungu, sisi ndio *hiki-na-hiki*.” “Mungu, sisi ni wa Umoja, haleluya, hao wengine wamekosea.” “Mungu abarikiwe, sisi ni Kanisa la Mungu la Unabii.” “Haleluya, sisi ni *Fulani-fulani*.” Vema, endeleeni. Walifanya nini? Waliendelea kubishania fundisho lao, mpaka wakakaa hapo mpaka walipokufa. Na hilo ndilo lililotukia sasa hivi, wamekufa, wamekufa pamoja na madhehebu yao.

¹³⁰ Nitamleta mwanatheolojia yeyote kwenye. . . kusema jambo hili, mwanahistoria, ninawajua wawili wazuri wanaoketi papa hapa sasa, hodari kama walivyo katika taifa hili, ninamwomba mwanahistoria yeyote kuniambia ya kwamba wakati wowote ambapo Mungu aliwahi kutenda kazi katika uamsho, ishara za kimbinguni zilifuata. Ni lini Yeye alipowahi kutenda kazi, ambapo mambo ya kimbinguni hayakufuata? Na ni lini walipoliundia hilo dhehebu, pasipo hilo kufa, wala halikuinuka tena? Nionyeshe wakati mmoja ambapo dhehebu liliwahi kuinuka likarudia asili yake tena. Lilikufa mara lilipounda dhehebu, vivyo hivyo na Wapentekoste.

¹³¹ Wale wapiganaji wa kale huko nje, wanaotaka kusema, “Haleluya, hatuna uhusiano wowote na hoja hiyo jipya, Utukufu kwa Mungu, tumepewa hiyo kwa unabii, haleluya, hatutakuwa na uhusiano wowote na Waassemblies wala wa Umoja, mojawapo, haleluya, sisi ni tofauti,” wao wamekufa. Hawachezi hata kidogo. Nao wamekufa, wametiwa alama, X. Alikaa pale na kuwaacha wafe, mpaka wakafa fofofu.

¹³² Ilikuwa ni kitu gani? Siku moja alikuja mmoja kutoka miongoni mwao, akasema, “Haya si yote yaliyoandikwa Hapa.” Wangepanya nini? Moja kwa moja kurudi kwenye uwanja ule ule wa kale kila usiku, wakizungukazunguka, kuuzunguka mlima huo, wakazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, maskini kitu kile kile, “Matendo 2:4, Matendo 2:4, Matendo 2:4, Matendo 2:4! Haleluya! Pokea Roho Mtakatifu, nena kwa lugha, Roho anakujalia kutamka. Utukufu kwa Mungu! Niombeeni kwamba niwe wa mwisho... yule ambaye Mungu amemwita katika siku hizi za mwisho. Matendo 2:4! Nina furaha nina Roho Mtakatifu akinena kwa lugha.” Hiyo ni kweli, hiyo ni sawa. Lakini kwa nini unasafiri kwenye mlima uu huu wa kale wakati kuna Nchi ya Ahadi mbele yako?

¹³³ “Mungu abarikiwe, nilijiunga na Assemblies.” “Nilijiunga na Umoja.” “Nilijiunga na *hili*.” “Nilijiunga na *lile*.” Kitu kile kile tu cha kale cha Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Katoliki, Lutheri, na hao wengine wamekwisha, walikufa njiani mwao, walikufa.

¹³⁴ Hilo ni gumu, najua, ndugu, ni kama kunywa mafuta ya mbarika, bali yatakufaa. Hiyo ni kweli. Kile kanisa linachohitaji siku hizi ni dozi nzu—nzuri ya dawa ya Injili, kukuondolea uvivu, kutoka kwako, ulimwengu, uchafu. Tunachohitaji siku hizi ni kurudi kwa nguvu za Roho Mtakatifu, kuongozwa na Roho.

¹³⁵ Ilikuwa ni kitu gani? Hicho kilikuwa ni kivuli na mfano wa kanisa la Kipentekoste siku hizi, miaka arobaini baadaye hapa tunajikuta tungali kwenye Matendo 2:4. Mungu huenda akaingia na kitu kingine, pamoja na baraka Zake zaidi, nao waseme, “Utukufu kwa Mungu, hatukuwa na hizo. Haleluya! Tunaamini Matendo 2:4. Vema, hapa, babu zetu waliunda *hili*, kama hawafikii *hili*, Mungu abarikiwe, hatuta—hatutashirikiana nao.” *Hummm, hummm, hummm!* Enyi maskini mliopotoka, *mliorudi nyuma!* Kuna shida gani? Wenye mashaka!

¹³⁶ Mnawezaje kumfuata Mungu? Mnawezaje kwenda mahali Roho aendako? Dhehebu lenu lingekuwa sawa kama mkimalizia fundisho lenu kwa koma, “Tunaamini *hili*, pamoja na yale Mungu anayoweza kuongezea kwalo.” Lakini mnamalizia kwa nukta, “Tunaamini *hili*, nawe ufuatae nyayo za *hili*, la sivyo hamna lingine.” Hivyo ndivyo Luther alivyofanya, hivyo ndivyo Wesley alivyofanya, hivyo ndivyo John Smith alivyofanya, hivyo ndivyo Alexander Campbell alivyofanya, hivyo ndivyo wote walivyofanya, na hivyo ndivyo Pentekoste ilivyofanya. Haya basi, umekufa miaka arobaini njiani mwako, nayo Nchi ya Ahadi ya utimilifu wa baraka za Mungu iko moja kwa moja mbele zako.

¹³⁷ Nini kilitukia? Siku moja maskini Yohana, aliamini kila Neno alilosema Mungu, hiyo ni kweli, akasema, “Yote ni kweli, Mungu alitushughulikia na kutimiza ahadi Yake, Yeye alisema angetupa mahitaji yetu wakati tukiwa huku nje, lakini hayo

si yote, kuna nchi ya ahadi, hebu tuiendee. Mmekuwa kwenye mlima huu miaka arobaini, geukeni sasa, kisha mgeuke upande wa kaskazini, na kupanda juu, kisha mvuke.” Amina.

¹³⁸ Kanisa la Kipentekoste limesimama katika madhehebu yake kwa muda wa miaka arobaini, mmekuwa hapa muda mrefu kutosha, ndugu, hebu tuinuke twende kaskazini, tuvuke Yordani, mahali ilipo nchi ya ahadi, ambako Mungu aliahidi kwamba “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Baraka na kila kitu alichohidi ni kwa ajili yetu, kila ahadi katika Kitabu hiki ni yako. Lakini inakubidi kufanya nini? Njoni Yordani kwanza, mkazifie kanuni zenu za imani na madhehebu yenu, mvuke.

¹³⁹ Kumbukeni, Yeye alisema, “Sasa, mnaposafiri, mnapanda kwenda kule kwenye mipaka. Sasa,” kasema, “msimguse Esau. Sasa, Esau ni Mlima Seiri.” Kasema, “Msimguse.” Kasema, “Nilimpa hiyo. Kama mkipitia huko, kama ninyi—kama mkila chochote, kilipieni, mkinywa maji yoyote, yalipieni, mumlipe. Msimguse mwaminio mkwamia mpakani, kwa sababu sitawabariki katika jambo hilo.” Mnaona? “Msimpige tena, piteni tu kimya kimya.”

¹⁴⁰ Sasa, kama Wamethodisti na Wabaptisti wanaishi huko juu mpakani... Kila uamsho uliowahi kutokea ulizaa mapacha, sijali ulikuwa wapi, unazaa mapacha. Mmoja wao... Ni kama tu—kama tu Esau na Yakobo, wote wawili waliwakilishwa katika hao wana wa Isaka. Esau alikuwa mtu wa ulimwengu, alikuwa mtu wa kidini, alishughulikia mambo, na kumshughulikia baba yake, naye alikuwa mtu mzuri. Lakini Yakobo alikuwa na upambanuzi, alijua ya kwamba haki ya mzaliwa wa kwanza ilimaanisha kila kitu, haikuleta tofauti yoyote jinsi ilivyombidi kuipata, bora tu aipate; huyo ni yule mtu wa kiroho siku hizi.

¹⁴¹ Huyo hapo Esau, alikuwa na urithi wake pale pale mpakani. Ndipo Mungu akamwambia, akamwambia Yakobo alipokuwa akipita, kasema, “Usijipumbaze na Esau, usijiunge na lolote la madhehebu yake, usifanye lolote la mambo haya hapa. Sasa, tayari umeona kile umekuwa nacho mwenyewe huku chini kwa miaka arobaini, kwani unataka kukaa miaka mingine arobaini?”

¹⁴² Ninyi ndugu, mnataka kutumia miaka mingine arobaini katika vurugu za kimadhehebu, mkizozana na ndugu yenu? Hebu tuinuke, na tuvuke, hebu tuende kwenye Nchi ya Ahadi, ambako kila ahadi katika Kitabu ni mali yako. *Yordani* maana yake ni “mauti,” huna budi kufa kwa nafsi yako kabla hujavuka. Hiyo ni kweli. Nenda kule. Watu wanaishi katika hali ya uvuguvugu, Biblia ilisema hivyo.

¹⁴³ Hao ndugu huko nje mlimani, wao—wao walibarikiwa, walikuwa... walifanikiwa. Vema, walikuwa na chakula kingi, mana ilianguka kutoka Mbinguni, hiyo ilikuwa ni sawa, bali

wangali walikuwa nje ya ahadi. Kama tu vile kanisa la Laodikia, wakati wa kanisa la Kipentekoste, wana baraka, bali Mungu hakujishughulisha nao, asingeweza kuwapeleka kwenye Nchi ya Ahadi, maana hawakuwa wametimiza masharti ya kwenda, mpaka walipofikia mahali ambapo walitambua walikuwa wamekufa katika nadharia zao, ndipo Mungu akawavusha.

¹⁴⁴ Sasa, alipopitia karibu na mlima wa Esau, akapitia karibu na hilo dhehebu, alifanya nini? Sasa, kulikuwako na Moabu, hakika, Moabu walikuwa ni dhehebu, kasema, “Utapita katika nchi yake, usi—usimwambie neno, nilimpa hiyo.”

¹⁴⁵ Sasa, Yeye aliwapa Wamethodisti mahali pao, akawapa Wabaptisti mahali pao, Yeye aliyapa madhehebu ya Kipentekoste mahali pao, msiseme neno kwao, piteni tu moja kwa moja, na kusema, “U hali gani, Ndugu? U hali gani?”

¹⁴⁶ “Lakini Yakobo, tuko njiani kuelekea Yordani.” Amina. Njiani mwetu kwenda Yordani! Kama wakisema, “Vema sasa, sikilizeni, kile . . .?”

¹⁴⁷ Vema, haiteti tofauti yoyote yale wanayosema, unasema, “Asante, Ndugu. Mungu awe pamoja nawe, Ndugu.” Pita tu kimyakimya, usiseme chochote, bali endelea kuelekea Yordani, maana tunapanda kwenda kuichukua Nchi ya Ahadi, tumepewa Hiyo, utimilifu wa nguvu za Mungu. Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.”

¹⁴⁸ Watu wanajaribu kushangaa ni kwa nini maono, na mambo makuu yenye nguvu hayatendeki kanisani, na uponyaji mkuu zaidi, na kadhalika, Mungu anataka kulivusha Kanisa, nasi tumerudi hapa chini kwenye mlima huu, tukizunguka, tukizunguka. Mlima wa aina gani? Mlima wa dhehebu. “Loo sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham, unapata . . .” Loo, la, sivyo nilivyo.

¹⁴⁹ Mlima Seiri, mlima, ulikuwa mali ya Esau, dhehebu lake kuu, nao Israeli wakajiundia mlima. Walikuwa mlimani, pia, lakini siku moja Mungu akasema, “Ondokeni kwenye mlima huu, nitawapeleka kule uwandani. Hamwezi kupata chochote kwenye milima hii ya kale ya mawe hapa, hamwezi kufanikiwa, nendeni kule, ambako ninaweza kuwabariki kwa maziwa na asali, na kuwamiminia mambo mazuri ya Mungu, na kuwatuliza.”

¹⁵⁰ Hilo ndilo Kanisa linahitaji usiku wa leo, ni kuondoka kwenye mlima huu, na kuelekea kaskazini, hebu tuachane na hali hizi baridi, za kawaida. Ninyi ndugu wa Assembly, ninyi ndugu wa Umoja, ninyi ndugu wa Church of God, ninyi nyote ndugu, hivi hatujakuwa hapa muda mrefu kutosha? Hebu tusahau tofauti zetu, hebu na tuweke mioyo yetu pamoja, mikono yetu pamoja, jitihada zetu pamoja, nia zetu, malengo pamoja, na twende mpaka Yordani, na kusulubiwa kwa ajili ya mambo haya, na tuvuke tuingie kwenye Nchi ya Ahadi, ambako

Mungu aliahidi kutembea pamoja nasi, na kutubariki, na kutupa mambo mengi kwa wingi sana.

¹⁵¹ Huwezi kuvunja mifano na vivuli vya Mungu. Hivyo ndivyo Israeli walivyofanya katika mambo ya kawaida, hivyo ndivyo wamefanya katika mambo ya kiroho. Tunatambua ya kwamba mambo hayo yalitendeka kwa Israeli, sasa yametendeka kwa kanisa siku hizi, kama tu yalivyotendeka wakati huo. Tuko karibu na mwisho wa safari sasa, ndugu, wakati umewadia kwa jambo fulani kutukia.

¹⁵² Ninataka kuvuka Yordani, nanyi je? kuingia kwenye Nchi ya Ahadi, ambako tunaweza kuona . . . Tumeona mambo mazuri, Mungu amekuwa mwema kwetu, hatulalamiki. Niko hapa nje pamoja nanyi, niko hapa nje juu ya mambo haya pamoja nanyi, lakini, ndugu, hebu na tujiweke pamoja, na tuvuke, lazima tuvuke.

¹⁵³ Yule Yoshua mkuu, Roho Mtakatifu aliyepokea ahadi kutoka kwa Mungu, aliyeshuka kuja kutuongoza, Yeye hajawahi kulitilia shaka. Yoshua kamwe hakulitilia shaka, alikuwa jemadari wa Mungu, hiyo ni kweli kabisa, yeye alikuwa jemadari wa Mungu, naye ndiye aliyewaongoza wale wana.

¹⁵⁴ Na ni Roho Mtakatifu yeye yule, Jemadari wa Mungu, yule Jemadari Mkuu aliyesimama kwenye malango ya Yeriko wakati Yoshua alipokwea, Kapteni Mkuu yule yule, Jemadari wetu, anataka kutuongoza kuingia kwenye Nchi ya Ahadi, na Yeye Ndiye pekee anayeweza kufanya hivyo. Madhehebu yetu hayatafanya hivyo, BWANA ASEMA HIVI. Andikeni hilo. Liweke tu hilo katika kitabu chako, uone kama hilo lilikuwa ni kweli au la. Madhehebu hayatakuwusha kamwe, yatakuweka papo hapo mlimani, bali Roho Mtakatifu atakupeleka kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁵⁵ Loo, hivi hamumpendi? Hivi hamumwamini? Hivi hamtaki kumtumikia? Loo, hayo ndiyo makusudi ya moyo wangu, ikiwa ninaujua.

¹⁵⁶ Bwana, jalia nimwone Yesu, jalia nimwone Yeye pekee. Hebu niende nikamlete kila ndugu wa Assembly aliyepo, hebu niwaendee na kuwachukua ndugu wa Umoja, hebu niliendee nilichukue Church of God, hebu niwaendee na kuwaleta ndugu hawa wengine wote, wowote wale, na kusema, “Ndugu, ndugu, na tuuache mlima huu!”

¹⁵⁷ Njoni Assemblies of God, njoni Church of God, njoni ninyi wa Umoja, Uwili, na chochote mliche, hebu na tuweke mioyo yetu pamoja, siku za vita zimekwisha, hebu tutembe taratibu kuelekea Kanaani. Haleluya!

Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba
ninasimama, (usiku wa leo, kwa imani,
Na kutupa jicho tamanifu,

Kwenye Nchi nzuri na yenye furaha ya
Kanaani,
Ilipo mali yangu.

Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?

Ninaelekea kwenye Nchi hii ya Ahadi.

¹⁵⁸ Kama itachukua kila kitu kilicho maishani mwangu, kila rafiki, kila kitu kingine, ninaelekea kwenye nchi ya ahadi. Je, unataka kwenda? Unataka . . . ? Hebu na tusimame kwa miguu yetu basi, kwa muda kidogo tu.

Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba
nasimama,
Na kutupa jicho tamanifu,
Kwenye Nchi nzuri na yenye furaha ya
Kanaani,
Ilipo mali yangu.

Inueni mikono yenu sasa mnapouimba.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;
Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

Kote juu ya zile nyanda pana tambarare
Huangaza Siku moja ya Milele;
Mahali ambapo Mungu Mwana milele
anatawala,
Na kuutawanya usiku.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;
Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁵⁹ Hatutaki kitu chochote kituongoze. Mungu Mwana milele anatawala, na kuvitawanya vitenga-ushirika vingine vyote. Loo, tunataka kukutana Naye. Hivi hutaki kumwona?

¹⁶⁰ Sasa, ninyi wa Umoja, wa Uwili, wa Utatu, Wamethodisti, Wabaptisti, Waassemblies, na ninyi nyote, peaneni mikono tunapouimba huo, peaneni mikono nyinyi kwa nyinyi, na kusema, "Mungu akubariki, ndugu, niko njiani kuelekea kwenye Nchi ya Ahadi."

Ninaelekea kwenye . . .

Geukeni moja kwa moja, peaneni mikono.

. . . Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;

Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁶¹ Loo, si inakufanya ujisikie vizuri zaidi? Hebu niwaonyeshe, nilikuwa katika moja ya madhehebu yetu maarufu yapata majuma matatu yaliyopita, ama manne, ilikuwaje? Nilifanya wito wa madhabahuni, wenye dhambi wanne ama watano wakaja madhabahuni. Nilipofanya hivyo, nikasema, “Je, mtu fulani atakuja na kuwaombea watu hawa?” Katika kanisa la Kipentekoste, hakuna mtu aliyekuja. Nikasema, “Je, baadhi yenu watakatifu mnaweza kuja na kuomba?” Nilikuwa nimechoka, nikasema, “Je, baadhi yenu watakatifu mwaweza kuja mkawaombee watu hawa?” Mnajua nini? Nisingeweza kuwashawishi kuja.

¹⁶² Ah, loo, ndugu, miaka arobaini iliyopita mmoja wao angalianza kuelekea madhabahuni, kungekuwako na watu hamsini karibu nao kabla hawajafika pale; mioyo yao ilikuwa inawaka moto, mnaona.

¹⁶³ Ati mnazungumza juu ya Wabaptisti? Nitawapeleka hapa katika jimbo la Kentucky, kwenye maskini lile Kanisa la Baptisti ya Kimishenari huko nyuma, nao si baridi tu, wa kawaida, kama baadhi yenu Wabaptisti wa kaskazini, wao hushuka madhabahuni, wanapigana mgongoni, mpaka watakapopita, wanacho kitu fulani kule chini. Naam, bwana.

¹⁶⁴ Nami nilikuwa huko chini si muda mrefu uliopita, kwenye Mapambo ambapo nyanya yangu, na wote hao wamezikwa kule chini, nami nilikuwa nikihubiri juu ya kuja kwa Mungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu; hao wanawake wakongwe wakizizungusha maskini hizo kofia za jua, na kupaza sauti. Huko nyuma kwenye vilima hivyo ambako hata hawawezi kuona, huwezi kupata gari umbali wa maili thelathini huko, huko nyuma ubavuni mwa vilima kule, wazee wakipaza sauti, wanawake, wakienda huku na huku sakafuni, wakimsifu Mungu.

¹⁶⁵ Basi alikuwapo maskini mvulana mkubwa, nilifanya wito wa madhabahuni, Nikasema, “Huyo hapo maskini nyanya yangu mkongwe huko nje kaburini, ambaye alifia mikononi mwangu akimsifu Mungu.” Nikasema, “Yule pale maskini shangazi yangu aliyenibusu shavuni katika saa ya kufa kwake, na kusema, ‘Billy, nitakutana nawe ng’ambo ya mto, huko ng’ambo.’” Nikasema, “Huyo hapo amelala, akingojea ile asubuhi ya ufufuo. Haleluya!” Nikasema, “Kama mmoja wenu hapa ni mwenye dhambi, ingia, Yesu anakualika.”

¹⁶⁶ Maskini mvulana huyo amesimama pale na kofia yake, akiitafuna nchani mwake, namna *hiyo*, akatupa kofia yake chini, kasema, “Mungu, unirehemu, mwenye dhambi!” Kulikuwako na ishirini wa mama hao wakongwe wamemzunguka kabla hata hajafika madhabahuni.

¹⁶⁷ Yapata ishirini ama thelathini wakakimbia kuzunguka madhabahu pale, wenye dhambi wote wakakimbilia mle ndani (Nasi tulipaswa kula chakula cha jioni saa tano, nasi tukala yapata saa tisa na nusu alasiri hiyo.), tukilia, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu, na kutembea huku na huku msituni wakipaza sauti na kumsifu Mungu. Nena kuhusu Pentekoste! Ilikuwa katika Kanisa la Baptisti ya Kimishenari.

¹⁶⁸ Nikaja moja kwa moja hapa kwenye kanisa la Kipentekoste, nao wenye dhambi wakimiminia mioyo yao madhabahuni, na hata nisingeweza kumshawishi, kama mtumishi wa Kristo, mtu fulani aje apige magoti karibu nao. *Whiu!*

¹⁶⁹ Hivi nimerukwa na akili? Je, nina kasoro? Nilimwuliza mke wangu, nikasema, “Mpenzi, niambie kuna nini?” Nilimwuliza Ndugu Moore, wahudumu, “Mimi, hivi nimeingia kichaa? Je, hi—hili Neno...? Kuna shida gani? Hivi elimu nyingi kupita kiasi, kama vile Agripa alivyomwambia Paulo, zimenitia wazimu?” Nikasema, “La, bwana. La, bwana. Mtu fulani hana budi kulitetea.”

¹⁷⁰ Mhudumu mashuhuri, maarufu aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, ninakuamini wewe kuwa ni mtu wa Mungu, lakini hebu niweke mikono yangu juu yako, na kukuombea. Unawakosoa watu kupita kiasi.”

Nikasema, “Ndugu, unaamini kwamba ni kweli?”

Akasema, “La, lakini hiyo si kazi yako.” Kasema, “Kazi yako ni, kuwaombea wagonjwa.”

¹⁷¹ Nikasema, “Upuuzi! La, bwana. Mungu hatoi karama kuninii tu, kuwabembelezea wapate samaki na mikate. La, bwana. Yeye anawapa vipawa kutangaza uhuru, na kuhubiri Injili.” Sawa. Nami nikasema, “Nisipofanya hivyo, ni nani?” Nikasema, “Huwezi, kwa sababu una mipango mingi sana ya kuunga mkono. Sina kitu cha kuunga mkono ila Biblia yangu, na Roho Mtakatifu anayehubiri.”

¹⁷² Haleluya! Utukufu kwa Mungu! Nina furaha kuwa Mpentekoste, ninataka kila mtu ajue kwamba mimi ni Mpentekoste, nilimpokea Roho Mtakatifu. Si dhehebu la Kipentekoste, hilo liko mbali nami, mimi ni Mpentekoste kwa tukio. Yesu Kristo ni Mwokozi wangu, ninampenda. Hakuna kitu ndani yangu...

¹⁷³ Mtu mmoja mashuhuri wa dhehebu kubwa, alisema, “Ndugu Branham, kama tu utapatana juu ya mambo machache, tutakupeleka hadi kwenye vituo vikuu—vituo vikuu sana vya ulimwengu kwa ndege zetu, na kukuacha uhubiri, kama tu utakuja na kujiunga nasi.”

¹⁷⁴ Nikasema, “Jionee aibu! Mtu mwenye hadhi na heshima na digrii ya udaktari, angemwomba mtumishi wa Mungu kupatana juu ya Neno Lake!” Nikasema, “Kama nimekosea, basi

chukua Maandiko, unionyeshe mahali nimekosea.” Nikasema, “Mungu... Ungeweza kufanya jambo kama hilo, Ndugu?”

¹⁷⁵ Akainamisha kichwa chake, akasema, “Ninaamini wewe ni mtu wa Mungu.” Kasema, “Mke wangu angalikufa miaka kadhaa iliyopita.” Alikuwa mgonjwa mbaya sana wa kansa niliyepata kuona. Kasema, “Ulimtaja, na kumwita kwenye kusanyiko namna hiyo kwa Roho Mtakatifu.” Kasema, “Ninaamini.”

¹⁷⁶ Nami nikasema, “Halafu unaniomba nipatane? Hilo halipigi kwenye mishiya yangu. La, bwana. Nitadumu na Neno kama nikifa mimbarani.” Hivyo ndivyo baba zetu walivyofanya jambo hilo, kudumu kwenye Neno la Mungu, haidhuru kama ikikuchuna ngozi, na kukuambua ngozi, kaa hapo kwa vyovyote vile.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;
Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;
Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁷⁷ Nashangaa, katika ukimya, huku muziki ukipigwa, tafadhali, Dada, *Ninaelekea Kwenye Nchi Ya Ahadi*, je, kuna mwenye dhambi humu ndani ambaye hajui lolote kuhusu hili, ninalozungumzia, bali hata hivyo unaamini kwamba ni kweli, ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, kwamba ghadhabu ya Mungu ilimwagwa juu Yake, Naye akafa pale Kalvari, kifo cha mwenye dhambi, kupachukua mahali pako? Yeye alikufa kifo chako pale Kalvari, na ni katika Yeye tu unaweza kuokolewa, wala hujafanya hivyo bado, nitawaalika kwenye madhabahu hii. Njoni hapa sasa, mkapatanishwe pamoja na Mungu kwa njia ya Kristo.

¹⁷⁸ Kama wewe ni mfuasi wa kanisa, hujui chochote ila dhehebu lako, ingawa huenda likawa ni Pentekoste, ingawa huenda likawa ni Methodisti, Baptisti, Katoliki, Othodoksi ya Kiyahudi, Kiyunani, lolote uwezalo kuwa, wala hujui chochote ila dhehebu lako, hujawahi kukutana na kitu fulani, kuzaliwa upya ambako kumekubadilisha, na kukufanya hai, bila kupatana na mambo ya ulimwengu, hutaki uhusiano wowote na ulimwengu, hutaki uhusiano wowote nao, umekufa kwake, nawe unataka kuwa hai katika Kristo, kama hujapokea tukio hilo bado, je, utakuja hapa madhabahuni, tunapoimba tena?

¹⁷⁹ Kama huna Roho Mtakatifu, nawe unataka kumpokea Roho Mtakatifu, je, utakuja madhabahuni, na kusimama hapa

tunapoimba tena? Ninyi wasafiri wote mnaotaka kujiunga nasi, na kwa imani, na neema ya Mungu mwelekee kwenye Nchi ya Ahadi, imbeni pamoja nami sasa. Vema.

Ninaelekea kwenye ninii ya Ahadi . . .

Ninawaalika, "Njoni," hilo tu ndilo ninaloweza kufanya.

Ninaelekea kwenye ninii ya Ahadi . . . (Mungu akubariki, Ndugu.)

Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

Ninaelekea . . . Nchi ya Ahadi,

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;

Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

Nitauona lini uso wa Baba yangu,

Na kupumzika kifuani Mwake?

¹⁸⁰ Ninataka kuwaambia, wakati tukiimba wimbo huu, ninii . . . Nilikuwa nimesimama, watu mia tano huko Jeffersonville, miaka thelathini na mmoja iliyopita, uamsho wangu wa kwanza, nikiimba, "Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba ninasimama, na kutupa jicho tamanifu, kwenye Nchi nzuri na yenye furaha ya Kanani, ilipo mali yangu," nami nikatoka nje, nikibatiza watu mia tano alasiri hiyo, kama mhubiri wa Baptisti ya Kimishenari, mtu wa kumi na saba niliyembatiza, mara nikasikia *Kitu fulani* kikisema, "Angalia juu," ndipo nikaangalia, na hii hapa ikaja ile Nguzo ya Moto ikizunguka kutoka Mbinguni, ikasimama papo hapo nilipokuwa, na kusema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia Kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia Kuja mara ya pili kwa Kristo."

¹⁸¹ Wakati yule mhubiri wa Kibaptisti aliponicheka . . . Hiyo iliandikwa kwenye *Associated Press, Nuru Ya Ajabu Yatokea Juu Ya Mhudumu Huku Akibatiza*. Kote kuingia huko Canada, na kwingineko kote ilikoenda kwenye *Associated Press*, mamia na maelfu ya watu waliiona. Iangalie leo, ndugu, angalia, ahadi Yake ni ya kweli. "Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba nasimama, na kutupa jicho tamanifu!" Tumekuwa katika nyika hii muda mrefu kutosha, hima twendeni kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁸² Hapa limesimama kundi la watu hapa wakimtafuta Mungu, wakimtaka Mungu, wakitaka kwenda kwenye Nchi ya Ahadi. Nashangazwa sasa, na baadhi yenu wahudumu, baadhi yenu ndugu ambao mna mzigo moyoni mwenu kwa ajili ya nafsi iliyopotea, mtasimama hapa pamoja nao.

¹⁸³ Ninyi mnaotaka bado kumpokea Kristo, mtakuja, mje huku, pia? Simameni kuizunguka madhabahu. Hawa wanaume na

wanawake, wavulana kwa wasichana wako hapa kumpokea Kristo kama Mwokozi wao. Mkitaka... Huku tukiimba tena, “Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba ninasimama, na kutupa jicho langu tamanifu.”

¹⁸⁴ Musa alisimama pale juu, na kuangalia katika nchi ya ahadi, madhehebu, alikatazwa kwenda kwa sababu alimkosea Mungu, lakini Yoshua alichukua vyombo vya Mungu na kuingia katika nchi ya ahadi. Neema ya Mungu itatupitisha, ndugu.

... za Yordani zenye dhoruba nasimama,
Na kutupa ninii tamanifu...

Je, mtakuja, vijana, wazee, yeyote yule, kujiunga na...?

... nchi nzuri na yenye furaha ya Kanaani,
Ilipo mali yangu.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi;
Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?
Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁸⁵ Sasa, kila mtu awe na kicho kwa dakika moja, ninataka kuzungumza na watu hawa hapa.

¹⁸⁶ Marafiki zangu wapendwa, usiku wa leo ilibidi *Kitu fulani* kizungumze nanyi mpate kuchukua msimamo huu. Yesu alisema, “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Naye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Kuna aina moja tu ya Uzima usio na mwisho, Uzima wa Milele, na hiyo ni Uzima wa Mungu, Zoe. Kwa kuwa ulisimama kutoka kwenye kiti chako, na ukaja hapa, ilionyesha ya kwamba Roho fulani, miaka hii yote ambayo umekuwa makosani, *Kitu fulani* kilisimama karibu nawe usiku wa leo, na kusema, “Uko makosani,” huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu, “simama, njoo huku mbele,” nawe ukaja.

¹⁸⁷ “Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu.” Hiyo ni ahadi Yake, Yeye hawezi kuighairi, ni ahadi Yake, hakuna kuighairi. Yuko hapa apate kukupa... Kwa sababu kwamba umemtetea, Yeye atakutetea katika Siku hiyo. Yeye alipachukua mahali pako, sasa uko tayari kukubali ya kwamba umekosea, nawe unamjia Yeye upate rehema, hakuna kitu chochote unachoweza kufanya ila kumwamini Yeye, na kukubali kile Mungu amekuandalia, hicho ni wokovu.

¹⁸⁸ Kumbukeni, sikilizeni Neno Lake, Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Sasa, Mungu alikugeuza, hiyo ni sehemu ya Roho Mtakatifu aliyekugeuza; sehemu inayofuata ya Roho Mtakatifu ni kukutakasa, kukuondolea

uchafu wote; sehemu ya tatu ya Roho Mtakatifu ni kukubatiza katika Mwili, ndipo umejazwa na Roho Mtakatifu na nguvu za Mungu. Hiyo ndiyo sababu umesimama hapa usiku wa leo, kwa sababu unachukua msimamo wako wa kwanza kumpokea Kristo kama Mwokozi wako.

Sasa nataka kusanyiko wainamishe vichwa vyao.

¹⁸⁹ Baba yetu wa Mbinguni, watu hawa wanaosimama hapa wanayaonea aibu maisha yao ya zamani. Wamesimama hapa kwa sababu walisikia Sauti Yako ikisema kwamba walikuwa wamekosea, nao wamekuja kukuchukua Wewe kama Mwokozi wao binafsi. Wamesimama hapa chini ya hatua ya kuhesabiwa haki, “Basi tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Ninakuamini Wewe, Bwana, ninaamini Maneno Yako ni kweli, na ninaposimama, usiku wa leo, kama mtumishi Wako, mmoja wao, ambaye anawaombea watu hawa, nami ninawakumbusha yale Wewe uliyosema.

¹⁹⁰ Hawa hapa, walisimama kutoka kitini mwao na kusogea hapa juu, kwa sababu walishawishika ya kwamba Wewe ulikuwa ni Mwana wa Mungu, Nawe ulikufa kwa ajili ya dhambi zao, nao wanataka neema Yako inayosamehe. Lingekuwa ni jambo lisilowezezana kwao kutoipokea, Wewe uliahidi hiyo, ni yao, wanaiamini, wamekuja kuishuhudia. Ulisema yeye ambaye—ambaye atakuonea Wewe aibu mbele za watu, Wewe utamwonea aibu mbele za Baba, na Malaika watakatifu, “bali yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu.”

¹⁹¹ Bwana, wao ni Wako, walishawishika walikuwa wamekosea, walisimama hapa kwa Neno la Mungu kushuhudia ya kwamba wamekosea, na wanataka msamaha. Ninazitetea nafsi zao, Bwana, ninawakabidhi Kwako, Baba, wao ni tunu za Neno Lako lililohukumu maisha yao yenye dhambi, nao wamekuja kukukubali Wewe kama Mwokozi wao binafsi. Ninakusihi unipe ahadi Yako, nikikumbuka ya kwamba Wewe ulisema ya kwamba “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Sasa wanalikubali Neno Lako, wanasikitikia dhambi zao, na wameonyesha vivyo hivyo, na kulidhihirisha kwa kuchukua msimamo kwa ajili Yako, usiku wa leo.

¹⁹² Baba, ninaomba ya kwamba utawapa ubatizo wa Roho Mtakatifu, zitakase nafsi zao, na kuwafanya viumbe vipya katika Kristo. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Mwanao mwenye upendo, Yule aliyelipa gharama ya kuwakomboza, wao ni Wako, karama za upendo, Ee Mungu. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuwatoa katika mkono wa Baba Yangu, hakuna aliye mkuu kuliko Yeye,” nao wako mikononi mwa Mungu.

¹⁹³ Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na hawa wanaokuja madhabahuni, hakuna jambo unaloweza kufanya, sio lazima uhisi chochote, Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini?” Kweli unaamini sasa ya kwamba katika hali ya dhambi uliyokuwamo, kwamba wewe, *Kitu fulani* kilikushawishi kwamba ulikuwa makosani, ulikuja hapa juu ya msingi wa Neno la Mungu lililokuahidi, kama ungekiri dhambi zako, Yeye alikuwa mwenye haki kuzisamehe, nawe sasa unazikanusha dhambi zako na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako binafsi, kama mtaweza, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mwinue mikono yenu? Kila mmoja wenu madhabahuni, aliyesimama hapa, sasa mkubali Yeye kama Mwokozi binafsi. Asilimia mia moja, kila mmoja. Mungu ashukuriwe.

¹⁹⁴ Sasa, ninawatangaza ninyi Wakristo, waaminio, raia wenza wa Ufalme, katika Jina la Yesu Kristo. Nitawaomba mnifanyie jambo fulani, ninawatakeni, kile chumba kidogo pale, kinachosema *Chumba cha Maombi*, Ninawatakeni mpitie moja kwa moja upande *huu*, na mwende pale wakati nikitoa wito mwingine. Nendeni pale mwendelee kuomba, ambapo tutakutana nanyi, katika dakika chache tu. Nendeni pale, na kupiga magoti, na kusema, “Asante, Bwana Yesu, kwa kuiokoa nafsi yangu.” Ninaamini Mungu, papo hapo, atawajaza na Roho Mtakatifu, mumo humo chumbani. Nendeni moja kwa moja upande *huu*, wakati mmoja wa hawa ndugu akiwaongoza.

¹⁹⁵ Sasa, wakati hawa wakienda pale, na wakufunzi sasa, kwa ajili ya jambo hi—hili, ambataneni nao. Watu hawa walimkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi.

¹⁹⁶ Sasa, kwenu mnaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu, mtakuja mbele wakati *huu*? Njoni mbele sasa, tunapoimba mara nyingine tena, useme, “Ndugu Branham, nime mtamani Roho Mtakatifu kwa miaka mingi, lakini bado sijampokea.” Njoo hapa juu. Kama unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, kama unaamini ninakwambia kweli, njoo hapa, hebu nikuombee. Maombi hubadilisha mambo, hufanya viumbe vipya. Kama wewe ni mwaminifu sana, songa mbele sasa, tunapoimba.

Kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba
nasimama,
Na kutupa jicho tamanifu,
Kwenye Nchi nzuri na yenye furaha ya
Kanaani,
Ilipo mali yangu.

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi,

¹⁹⁷ Wote wasio na Roho Mtakatifu, ninawaita katika Jina la Kristo, njoni huku mbele.

Ee ni nani atakayekuja na kwenda pamoja
nami?

Ninaelekea kwenye Nchi ya Ahadi.

¹⁹⁸ Je, wewe ni mwaminifu? Je, hawa ndio wote walio kwenye jengo hili ambao hawana ubatizo wa Roho Mtakatifu? Ndugu, dada, unawezaje, chini ya presha kama hiyo ya Roho Mtakatifu, kufikia mahali ambapo huna Roho Mtakatifu, wala hutasimama kwa ajili ya maombi? Unawezaje kutarajia uponyaji wakati hata nafsi yako haitaponywa kutokuamini upate kumpokea Roho Mtakatifu? Utapokeaje uponyaji wa Kiungu kwa ajili ya mwili wako? Hivi hutakuja? Umealikwa. Ndugu, dada, raia wenzangu ambao tayari wamemkubali Kristo kama Mwokozi wenu, mnataka ubatizo wa Roho Mtakatifu?

¹⁹⁹ Vema. Ninataka baadhi yenu watu ambao ni watu wazuri, walio na Roho Mtakatifu, waje hapa, na kuweka mikono juu ya watu hawa, tunapowaombea. Njoni mbele sasa, weka mikono yako juu ya mtu fulani.

²⁰⁰ Huko nyuma, mlio na Roho Mtakatifu, baadhi yenu ndugu wahudumu, njoni hapa juu, muweke mikono juu ya watu hawa kama uwakilishi. Mungu akubariki, Ndugu Gene. Njoni moja kwa moja mbele, njoni moja kwa moja, ndugu. Njoni moja kwa moja hapa mkaweke mikono juu ya watu hawa, tunapoomba. Hilo ni jema. Njoo, Ndugu Fred, hilo ni sawa. Njoo moja kwa moja mbele. Haleluya!

²⁰¹ Baba yetu wa Mbinguni, watu hawa wanatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, wamechoshwa na zabibu hizi, wanataka maziwa, asali, wanataka kwenda kwenye Nchi ya Ahadi. Ninakuomba Wewe, Bwana, kwa moyo wangu wote, watu wanapowekeana mikono, kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba Wewe utawapa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Maombi ya imani yatafanya hivi, tunajua. Tunawakabidhi kwako, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

²⁰² Amina. Hiyo ni kweli. Wote wanaotaka uponyaji wa Kiungu, inueni mikono yenu, wote wanaotaka kuponywa, inueni mikono yenu. Sasa mtu fulani uweke mikono yako juu yao huko nje, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Sisi hapa. Ombeaneni. Tunaelekea kwenye Nchi ya Ahadi, kila ahadi ambayo Mungu alitoa.

²⁰³ Baba wa Mbinguni, hawa ni Wako, ninawakabidhi kwako, Bwana. Waponye wagonjwa, wajaze na Roho Mtakatifu wale wanaohitaji, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi sasa, katika Jina la Yesu...?...



61-0316 Kanisa Likichagua Sheria Badala Ya Neema
National Guard Armory
Middletown, Ohio Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org